# families worldwide

Nambari **26** Toleo **2.20**



## Kuchukua hatua kuelekea amani na maridhiano

Mothers' UNION
Christian care for families

SHAJARA YA MAOMBI:
JULAI - DESEMBA 2020











3 **Barua la Raisi wa kidunia**

4-5 **Ukanda wa A** Korea, Myanmar, India Kaskazini, India Kusini, Sri Lanka

6 **Ukanda wa B** Kanada, Marekani Kusini, Marekani, West Indies

7 **Ukanda wa C** Aotearoa, Nyuzilandi na Polynesia, Australia, Melanesia, Papua New Guinea

8 **Ukanda wa D** Kenya, Uganda, Rwanda, Tanzania, Yerusalemu na Mashariki ya Kati

9 **Ukanda wa E** Afrika ya Kati, Nijeria, Sudan Kusini, Sudan, Kusini mwa Afrika

10 **Ukanda wa F** Burundi, Kongo, Bahari ya Hindi, Afrika Magharibi

11 **Ukanda wa G** Canterbury (na Ulaya)

12 **Ukanda wa H** York

13 **Ukanda wa I** Irelandi Yote

14 **Ukanda wa J** Scotlandi / **Ukanda wa K** Wales

15-42 **Shajara ya Maombi:** Julai – Desemba 2020



*Families Worldwide* ni rasilimali ya kuongeza maarifa kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama, inayochapishwa mara mbili kwa mwaka na kusambazwa bure kwa wanachama na marafiki walio Uingereza na Ireland. Wanachama wa nchi za kigeni na marafiki wanaweza kupokea nakala ya PDF kupitia barua-pepe kutoka mikoa ya ndani.

*Families Worldwide* sasa imetafsiriwa kwa lugha za Kifaransa, Kihispania cha Amerika Kusini na Kiswahili.



**Andika barua kwa:** Mothers' Union, Mary Sumner House, 24 Tufton Street, London, SW1P 3RB

**T: 020 7222 5533**
**E: publications@mothersunion.org**
**www.mothersunion.org**



**Registered Charity Number: 240531**

**Rais wa kidunia:** Sheran Harper
**Mkurugenzi mkuu:** Bev Jullien

*Families Worldwide* imechapwa na Mothers' Union

**Mhariri:** Beth Lanksford

**Msimamizi wa machapisho:** David Baronti

**Kubuni:** Adam Austin

**Kimechapwa na:** Halcyon Print Management Ltd



Karatasi iliyotumika katika chapisho hili imetengenezwa kwa kutumia mbao kutoka misitu endelevu na ambayo haina klorini. Huku kila juhudi ikiwa imechukuliwa ili kuhakikisha usahihi wa tarehe na maoni, Ushirika wa Akina Mama hauwezi kukubali jukumu kwa hasara yoyote, uharibifu au usumbufu unaosababishwa kwa makosa yoyote au upungufu.

© hati miliki ya yaliyomo 2020

# Dada na ndugu zangu wapendwa,



Ninawaandikia kwa upendo na ujasiri wa Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wetu kwa sababu Yeye ndiye nguvu yetu, tumaini letu na mwamba wetu imara.

Mengi yamekuwa yakiendelea hivi karibuni kwani COVID-19 imetangazwa kuwa janga, na serikali zinashauri kwamba tuchukue tahadhari muhimu ili kuzuia kuenea kwa virusi. Kuna mengi sana ambayo tumelazimika kukubaliana nayo kwa muda huu mfupi.

Katika nyakati kama hizi, ninakutia moyo, na usiogope kwa sababu Bwana, Mungu wako yuko kando yako - msaada wako wakati wa shida. Katika Yoshua 1: 9 tunasoma, Kumbuka kuwa mimi nimekuamuru uwe imara na hodari. Usiogope wala usifadhaike kwa kuwa mimi Mwenyezi-Mungu, Mungu wako, niko pamoja nawe popote uendapo." Amina

Nyinyi kama wanachama ni wajasiri na shupavu; tena mmejazwa na ujasiri na huruma. Mna upendo mwingi na kama Esta, mnasimama mstari wa mbele kila siku mkitaka kukomesha ukosefu wa haki na kutetea yote yanayounga mkono familia na jamii zilizo imara.

Mmeshughulika katika vitendo hivi vya upendo lakini sasa wengi wenu wanaambiwa wanyamaze na kujitenga katika juhudi za kuzuia kuenea kwa virusi. Mtagundua ya kwamba bado kuna mengi tunayoweza kufanya kama washirika kwa sababu sisi kama harakati tuna uwezo mkamilifu wa kusaidia na kuchukua hatua wakati huu, tukifuata ushauri wa kiafya uliotolewa na serikali zetu.

*Families Worldwide* ni rasilimali bora ya kuongoza sala zako kwa ajili ya washiriki kote ulimwenguni na shuhuda zilizo kwenye taarifa za nyanda zinaweza kufungua mazungumzo mazuri. Ninakuhakikishia kwamba ukitumia chapisho hili utapata hisia za upendo na umoja.

Bwana Yesu Kristo,
Uliwaambia wanafunzi wako,
Nipo nanyi siku zote, hata hadi mwisho wa wakati
Kuwa na mimi leo, Bwana, wakati ninajitolea kwako.
Sikiliza maombi yangu kwa ajili ya wengine na yangu mwenyewe,
Na uniweke katika utunzaji wako wa upendo kila wakati. Amina.

Wako katika upendo na Maombi,

Sheran Harper
Raisi wa Kidunia

# Korea, Myanmar, India Kaskazini, India Kusini, Sri Lanka

**Mdhamini:** Roshini Mendis
**Idadi ya Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 1,915,369
**Idadi ya watu:** Bilioni 1.4
**Lugha kuu:** Kihindi, Kiberma, Kikorea na Kisinhali



Kufuatia MULOA,wanachama wa Ushirika wa Akina Mama nchini Myanmar, Sri Lanka na Korea sasa wanasikiliza vizuri jamii zao ili kuona mahitaji yao ni yapi hasa. Ushirika wa Akina Mama unaonyesha jamii ya kwamba ni kweli wanawajali. MULOA imewaonyesha kuwa tayari wana rasilimali wanazohitaji ndani yao wenyewe na jamii zao ili kukabiliana na changamoto zao.



*Wanachama wa Sri Lanka na India wakiomba katika warsha ya MULOA*

Kuwahamasisha akina mama wachanga kujiunga na Ushirika wa Akina Mama nchini Sri Lanka imekuwa ni changamoto. Sababu moja inahusu muda kwa sababu vijana hawa wana shughuli za kikazi na pia masomo ya watoto, jambo ambalo linaweza kuchukua wakati mwingi sana. Maisha kwao yamekuwa ni kama mbio ambayo inawaletea mfadhaiko. Huko Myanmar changamoto kuu inayokabilia wanachama ni hali ya kisiasa nchini. Wanachama hawawezi kuwafikia baadhi ya jumuiya kwa sababu wanatakiwa kupata kibali cha serikali ili kufikia maeneo hayo na wakati mwingine wanakosa kufanikiwa kabisa kupata ruhusa.

Kwangu binafsi, kama mdhamini kwa Kanda A, changamoto yangu kubwa ni kuleta Kaskazini mwa India katika jamii ya kimataifa ya Ushirika wa Akina Mama. Jumuiya ya Wanawake India Kusini wana mwamko mkubwa. Namsifu Mungu kwa hayo.

Katika Baraza la Kimataifa la mwaka wa 2019, tulikubaliana juu ya baadhi ya mambo yatakayopewa kipaumbele katika ukanda wetu na kuamua kuwa kazi yetu yote inapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

**1.** Elimu kwa watoto - katika nchi zetu kuna watoto wengi ambao huacha shule kutokana na ukosefu wa fedha na mahitaji ya masomo. Tunaposaidia watoto kama hao katika elimu yao, tunaurahisisha mzigo katika familia zao na pia tunawapa watoto msaada wa kimaadili. Wakiwa na elimu nzuri watakuwa na fursa ya kupata ajira.

**2.** Maisha ya wanawake – Kwa kawaida vijijini, wanaume ndiyo wenye mapato pekee na ndiyo wanatawala wanawake. Wakati mwingine akina baba hawajishughulishi na mahitaji ya watoto. Hivyo basi, wanawake wakipewa mafunzo katika ujuzi ili waweze kujipatia mapato yao, watashughulikia zaidi kutimiza mahitaji ya familia zao.

**3.** Waathirika wa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia- kuna waathirika wengi ambao huteseka katika ukimya kwa sababu ya unyanyapaaji wa jamii na pia kutokana na ukosefu wa makazi na msaada kwa waathirika hao.

**4.** Mabadiliko ya hali ya hewa - tunataka kuwaelimisha wanachama wetu kuhusu jinsi ya kupunguza matumizi ya plastiki na umuhimu wa kupanda miti, na kuwa mfano mzuri kwa kizazi cha vijana katika kutunza viumbe.

## Shuhuda za mabadiliko

Mradi wa UAM wa Mpango wa Ulezi huko Myanmar unaendelea vizuri. Jamii ya watu wa dini zingine ilijiunga na mpango huu na baadhi ya wazazi wameingia katika vikundi vidogo vya kuweka akiba ambavyo vinasimamiwa na UAM. Kupitia Mpango wa Ulezi, akina mama wamejifunza kuwa na subira zaidi na kujali watoto wao. Jambo hili limesababisha mabadiliko kwa watoto ambao sasa wanajiamini zaidi, na kuwapelekea kufanya vizuri katika masomo yao. Akina mama walisema kuwa hata uhusiano wao na waume zao umeboreshwa kutokana na Mpango wa Ulezi. Kupitia vikundi vidogo vya kuweka akiba, akina mama wameweza kutimiza mengi. Mama mmoja ameweza kujenga nyumba yake na sasa anaendesha biashara ya upishi nyumbani kwake. Alishukuru sana mpango huu.

# Kanada, Marekani ya Kusini, Marekani, West Indies



**Mdhamini:** Kathleen Snow
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 13,271
**Idadi ya Watu:** Milioni 832 **Lugha kuu:** Kingereza, Kifaransa, Kihispania, Wichi, Toba, Kiholanzi, Papiamento



*Mary*



*Kathleen na Jane*

MULOA imeleta mafanikio makubwa katika Ukanda B. Imewatia nguvu wanachama wetu wa Ushirika wa Akina Mama na kuwahimasisha wawe na mtazamo chanya katika huduma kwa jamii zao.

Mikutano ya pamoja ya wanachama kutoka mikoa mbalimbali katika ukanda wetu imeleta mafanikio chanya. Wanachama wanahisi kuwa na ushirikiano kati yao, na wamekuwa makini zaidi kuhusu kinachoendelea katika nchi za wenzao. Imewapa mtazamo zaidi wa kimataifa na kuwapa moyo wa kuungana na kusaidiana.

Katika Amerika ya Kusini wengi wa wanachama wa AMARE wanatoka kwenye jamii za kiasili. Jamii hizi ni maskini sana na mara nyingi kumekuwa na mifarakano katika mikutano. Hata hivyo, wamepata mafanikio makubwa katika kuanzisha katiba mpya ya AMARE, katiba ambayo itatoa muongozo wa utawala bora na muundo mpya wa utendaji kazi. Tumepata mkufunzi mpya wa Mpango wa Ulezi, Bi. Mechi Tarragona, ambaye ni mkwe wa Askofu wa Uruguay. Tunatarajia kupata maendeleo katika uanachama wa UAM nchini humo, pamoja na Paraguay.

## Shuhuda za Mabadiliko

Katika Jimbo la Jamaika na Visiwa vya Cayman, wanawake vijana wawili waitwao Maria na Jane * walishiriki katika Mpango wa Ulezi. Jambo hili lilimpeleka mwezeshaji kupata wazo la kuwaingiza kwenye ustadi wa mafunzo ambapo walipewa nafasi ya kufikiria juu ya vitu wanavyoweza kutengeneza wenyewe na kuviuza katika masoko ya mitaa. Mmoja alianza kufuma krochia na mwingine kutengeneza mapambo ya vito. Wote wamepata mafanikio.

Tangu wakati huo, waliweza kuomba na kupata ushauri kuhusu jinsi ya kujiandikisha na Jamaica Business Development Corporation (JBDC), na sasa wamepata kadi zao za biashara. Wanawake wote wawili watakuwa wakipata msaada na kukuza bidhaa zao kupitia “Things Jamaican”, ambayo ni biashara ya mfululizo wa maduka sita ya rejareja wenye lengo la kukuza maendeleo ya kazi ya mikono nchini Jamaika, kuvipa thamani vitu vitengenezwavyo kwa mikono katika kisiwa hicho katika kuchochea vitu hivyo kununuliwa zaidi.

** Majina yamehifadhiwa ili kulinda utambulisho*

# Aotearoa, Nyuzilandi na Polynesia, Australia, Melanesia, Papua New Guinea



**Mdhamini:** Libbie Crossman **Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 45,323 **Idadi ya watu:** Milioni 113
**Lugha kuu:** Kingereza, Kimaori, Kiniven, Solomon Island Pidgin, PNG Pidgin, Motu + Zaidi ya lugha za kiasili 700 za masiwani

Kanisa la Anglikana katika Mkoa wa Aotearoa, Nyuzilandi na Polynesia, ni cheo kamili ya Mkoa wa Nyuzilandi. Mkoa huu umeundwa kwa mikondo mitatu na kila mmoja una askofu mkuu wake; Aotearoa ni mkondo wa Maori; Nyuzilandi ni mkondo wa Ulaya na Polynesia ni kwa ajili ya Wapolinesia wanaoishi Fiji, Tonga, Samoa, Visiwa vya Cook na pia Wapolinesia ambao wamehamia Nyuzilandi. Kwa sasa hakuna wanachama wa Ushirika wa Akina Mama ninaowajua katika Visiwa vya Cook. Fiji, Tonga, Samoa na Visiwa vya Cook ni mataifa tofauti yalio na haki zao wenyewe. Mkoa wa kiAnglikana wa Melanesia una wanachama katika nchi tatu tofauti: Visiwa vya Solomon, Vanuatu na Kaledonia Mpya, walio na askofu mkuu mmoja. Australia na Papua New Guinea (PNG) si ngumu kuelewa - nchi mbili, mikoa miwili!

## Shuhuda za mabadiliko

Laura, mmoja wa washiriki wa MULOA kutoka PNG alikuja kwangu na kusema, "Hili limekuwa jambo zuri sana na nimejifunza mengi, lakini sijui kama nina uwezo wa kwenda nje na kuongoza semina ya MULOA".

Parokia yake iliulizwa kama baadhi ya wanachama wake wangeweza kusaidia katika sherehe inayohusisha kuandaa chakula cha jioni kwa ajili ya moja ya makampuni katika jamii hiyo. Laura aliweza kuelewa jinsi hili jambo lilihusiana na yale ambayo yeye alikuwa amesikia katika MULOA. Chini ya usimamizi wa Laura, washiriki wa kundi wakashona vitambaa vya meza, wakatayarisha na kuupamba ukumbi kwa maua na wakaandaa chakula. "Ilifana sana. Tulivaa sare zetu za UAM na watu kadhaa walitaka kujua UAM inahusu nini".

Wakati Laura aliwasili kwenye MULOA yake ya pili alikuwa na shahuku ya kutoa shuhuda yake. Mwenendo wake wote ulikuwa umebadilika. "Nilielewa kwamba ningeweza kufanya vile, niweze kuongea kuhusu Ushirika wa Akina Mama kwa jamii na ninajiamini kwamba naweza kusimamia na kutoa warsha".

Mumewe alisikia habari kuhusu sherehe, na sasa uhusiano wake na Laura umekuwa bora zaidi. Laura ameshakamilisha awamu yake ya ofisi katika UAM. Wakati wa makabidhiano - tukio kubwa katika PNG - mume wake alimwambia mumewe mrithi wa Laura amsaidie mke wake kwa sababu kwa kufanya hivyo itaboresha ndoa yao, na kwamba atakuja kujivunia mke wake.

# Kenya, Uganda, Rwanda, Tanzania, Yerusalem na Mashariki ya Kati



**Mdhamini:** Mary Kamwati
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 1,019,591
**Idadi ya watu:** Millioni 573 **Lugha kuu:** Kinyarwanda, Kingereza, Kiswahili, Luganda, Kiarabu, Kiyahudi

MULOA imekuwa na mafanikio makubwa katika ukanda wetu. Mawazo ya watu yamebadilishwa na wanachama wamejifunza kusikilizana, kuelewa changamoto za watu wengine na kisha kutenda kwa busara kwa mawazo yalio chanya. Jumuiya zimesaidika kwa ujumla badala ya watu binafsi tu. Ushirika wa Akina Mama unawafikia watoto na vijana kwa njia ya mashule, kwa kutoa mafunzo juu ya usafi na uhusiano. Pia wanatoa ushauri kwa wazazi katika jamii, hasa kuhusu masuala kama vile ndoa za utotoni.



*Waratibu wa UAM Uganda wameshika kadi za "Make a Mother's Day" za mwaka mpya wa 2020 zilizotengenezwa kwa kutumia mbegu*

## Shuhuda za mabadiliko

Huko Awor, Uganda, baadhi ya wanachama wa Ushirika wa Akina Mama walikuwa wakiishi katika nyumba za nyasi. Mara nyingi nyumba hizi zilishika moto katika misimu ya viangazi, na kuchoma chakula chote na mali. Wanachama walivunjika moyo kimwili na kiroho, kwa sababu moto huo ulikuwa unatokea wakati ambapo wanachama wangeweza kuuza bidhaa zao kwa bei ya juu. Kwa hivyo mapato yalipatikana machache tu katika msimu usio na mafanikio kwa sababu ya bidhaa kuchomwa.

Uamuzi ulitolewa miongoni mwa wanachama, wa kuunda vikundi vya ushirika nyumbani na kukusanya pesa ili kila mwanachama aweze kufaidika. Hadi sasa, nyumba tatu za paa za mabati zimejengwa kwa kutumia fedha hizo za mzunguko. Pia waliamua kusaidiana kutunza vitalu vya mashamba yao ili kuongeza mavuno na hii imewezesha wanachama kujifunza ujuzi mpya

# Afrika ya Kati, Nijeria, Sudan Kusini, Sudan, Afrika Kusini



**Mdhamini:** Thembsie Mchunu
**Wanachama wa Ushirika Wa Akina Mama:** 259,168
**Idadi ya watu:** Milioni 419 **Lugha Kuu:** Kiingereza, Nguni, Kireno, Dinka, Kiarabu, Shona, Yoruba, Abon



*Wanachama wakileta bidhaa za matumizi ya nyumbani*

Kusikiliza kumekuwa na jukumu muhimu, tena kulileta mafanikio makubwa miongoni mwa wanachama katika ukanda wetu tangu kuanzishwa kwa MULOA. Wanachama wamejifunza kusikiliza wengine kwa makini, kisha kutenda kulingana na yale ambayo wameyasikia. Ushirika wa Akina Mama sasa una uwezo wa kuhamasisha miundo ya serikali inayohusika, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kusaidia jamii zilizo na mahitaji. Jumuiya pia zinahimizwa kutumia ujuzi wao na pia rasilimali zao ili kuendeleza maisha yao.

Ajenda kubwa ya ukanda wetu ni kuanza kufanya kazi na Green Anglicans kwa kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuzuia / kujiandaa kwa ajili ya maafa ya asili. Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo (MEL) ni jambo jipya katika ukanda wetu na ni baadhi ya mambo yatakayopewa kipaumbele kwetu. Hapo awali, hatukuweza kukusanya kwa usahihi takwimu kuhusu maisha yaliyobadilishwa na mipango yetu. Hivyo basi hili ni jambo tunalotaka kuboresha zaidi.

## Shuhuda za Mabadiliko

Katika mkutano wa Ushirika wa Akina Mama katika Mkoa wa Eastern Cape, Afrika Kusini, kitengo cha wenye ulemavu katika idara ya Elimu away kuvunja moyo kuhusu msichana mwenye umri wa miaka minane, Sibabalwe Mene, ambaye alizaliwa mlemavu wa mguu ambao ulikuwa haukui.

UAM uliahidi kutoa msaada wa kifedha ili Sibabalwe awekewe kiungo bandia ili kurahisisha maisha yake na kumsaidia kujiamini zaidi. Pia walijishughulisha na manispaa, pamoja na Maendeleo ya Makazi MEC ili familia yake ipate makazi bora. Parokia moja katika Fort Beaufort huwa inachangia vyakula kwa familia kila mwezi.

Baada ya Sibabalwe kupokea mguu wake wa viungo bandia, furaha na matumaini vilirudi katika maisha yake. Sasa anaweza kucheza na watoto wengine wa rika lake.

# Burundi, Kongo, Bahari ya Hindi, Afrika Magharibi



**Mdhamini:** Marie-Pierrette Bezara
**Wanachama wa Ushirika Wa Akina Mama:** 56,599
**Idadi ya watu:** Millioni 204 **Lugha kuu:** Kifaransa, Kirundi, Kiingereza, Malagasi, Creole, Lingala, Kiswahili

Wanachama katika Ukanda wa F wamekuwa wakishiriki zaidi tangu MULOA na wametia nishati katika uhusiano wao na Mungu na kati yao. Uhusiano kati ya watu binafsi na familia umeendelea kustawi kwa upendo. Jamii zinaanza kufanya kazi pamoja ili kuleta mabadiliko Baadhi ya vikundi vya watu ambao walikuwa wametengwa na jamii zao sasa wanajitegemea zaidi kutokana na msaada wa miradi na mipango ya Ushirika wa Akina Mama.

Wanachama wameweza kushirikiana kati yao katika ngazi zote - tawi, kijimbo na mkoa. Wamekuwa wakikutana mara kwa mara, angalau mara moja kwa mwezi.

Changamoto kubwa katika eneo letu ni udhalimu. Kwa hivyo kukabiliana na jambo hili kutapewa kipaumbele mwaka wa 2020.



*Vetiver – Vetiver - Nyasi inayokua haraka ambayo hulinda udongo wakati wa mvua*

## Shuhuda za mabadiliko

Kila mwaka, nchi ya Madagascar imekuwa ikiathirika na vimbunga ambavyo vinaharibu kabisa jamii. Majanga haya ni pamoja na mafuriko na uharibifu wa nyumba, ardhi na mifugo. Kwa upande mwingine, kutokana na mabadiliko ya mazingira, maeneo mengine ya nchi yanateseka kutokana na ukame wa mara kwa mara, unaoathiri sana kilimo na maisha ya watu wanaojitahidi kuishi.

Waratibu wa Ushirika wa Akina Mama katika Maendeleo ya Jamii na ya Jimbo walipata mafunzo kuhusu ujenzi wa mbinu na udhabiti katika jamii hapo mwezi wa Julai 2018. Kwa sasa wanatekeleza mafunzo zaidi katika majimbo yao.

Katika jimbo la Mahajanga, jamii hukabiliwa na ukame na mafuriko. Dayosisi inashughulikia swala hili la utunzaji wa mazingira. Wamechagua nyasi maalumu iitwayo Vetiver, ambayo inakua haraka huku ikihifadhi udongo wakati wa mvua. Baada ya Vetiver kung’olewa, miti huwa inapandwa katika sehemu hizo hizo - hasa miti ambayo inarutubisha udongo na ambayo inahifadhi maji katika mashina yao. Miti hii pia itatumika kama vizuizi wakati wa vimbunga.

Huu ni mfano mmoja tu wa jinsi Ushirika wa Akina Mama unafanya kazi na jamii ili kuwaandaa kwa ajili ya majanga, na wakati huo huo kuendelea kusaidia familia kubadilisha maisha yao wenyewe.

# Canterbury



**Mdhamini:** Nikki Sweatman
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 26,900
**Idadi ya watu** Millioni 40 (Mkoa wa Canterbury), millioni 741 (Uropa)
**Lugha Kuu:** Kiingereza



*Sehemu ya siku ya "Metamorphosis Taster"*

MULOA imehamasisha wanachama kuhusha imani yao na uanachama wao kwa Ushirika wa Akina Mama. Inawawezesha wengine kuongoza vikao na tena kuwasaidia kuona majukumu yao kwa upana kuliko kuandaa mkutano wa tawi tu na kualika msemaji. Katika baadhi ya maeneo, imeleta mafanikio chanya katika uhusiano kati ya makanisa na UAM kwa sababu tunajihusisha na ushirika wa kanisa ili watu wote waweze kushiriki katika ukuaji binafsi na ukuaji wa kiimani.

Kuna juhudi halisia za ngazi ya chini zibadilishazo maisha. Juhudi hizo za moja kwa moja zinawasaidia watu tunaowasaidia kuona kwamba wanapendwa na kuthaminiwa. Jambo lingine la muhimu, ni misaada ya kifedha au kwa ajili ya shida za aina mbali mbali. Miradi muhimu amabayo tunatilia maanani mwaka huu ni utumwa mamboleo na Mabadiliko ya mfumo wetu katika Uingereza wa kuhamasisha kanisa na jamii.

Mambo yatakayopewa kipaumbele zaidi kwa mwaka wa 2020 ni kuendeleza wanachama ili wachukue majukumu ya uongozi (kuwawezesha na kuwatia moyo). Tunataka Ushirika wa Akina Mama upate kujulikana katika jamii, na kuonyesha kuwa mipango yetu ni ya thamani kubwa, hasa kwa wale ambao wangependa kujiunga nasi.

## Shuhuda za mabadiliko

Katika Dayosisi ya Canterbury wanachama waligundua kuwa msichana mmoja alianza shule ya sekondari bila sare za shule. Hii ilimsababisha msichana huyo kutoweza, au kukataa kuhudhuria shule. Pia alikuwa akimuhudumia mtu mmoja katika familia yake, jambo ambalo lilimuweka mbali na wenzake. Alijiona kuwa tofauti na asiye na thamani. Hivyo basi wanachama walitoa msaada wa kifedha ili kumsaidia kununua sare yake za shule (wakishirikiana na Action for Children).

Hii ilileta mafanikio makubwa kwa familia yake nzima na kumfanya ajihisi ya kuwa yeye ni "mtu wa kawaida" kutokana na kupata sare hizo mpya. Wanachama walimsaidia kuongeza kujithamini kwake kwa kuonyesha kwamba hata matendo madogo yanaweza kuleta manufaa makubwa katika masomo na mafanikio ya rika.

# York

**Mdhamini:** Catherine Hilton
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 18,025
**Idadi ya watu:** Millioni 16
**Lugha kuu:** Kingereza



istock.com/Boonyachoat



*Kutoa matumaini kwa wafungwa katika Dayosisi ya Durham*

MULOA imeleta athari chanya katika kufufua wanachama katika ukanda huu na imewezesha kuendelea na hata kufungua upya baadhi ya matawi katika Mkoa wa York. Hata hivyo, changamoto yetu kubwa inaendelea kuwa ya uanachama kupungua, na tuna idadi ndogo ya wanachama wanaoshiriki katika kazi zetu.

Ushirika wa Akina Mama unaleta mafanikio makubwa zaidi katika jamii zake kwa njia ya kushirikiana na mashirika mengine ili kutoa mahitaji mbalimbali. Mahusiano ya karibu katika Kanisa na jamii yanaendelea kuimarika.

Maendeleo ya uongozi ni moja ya vipaumbele vyetu vikuu kwa mwaka 2020 kwa sababu ni muhimu katika mustakabali wa maendeleo ya harakati za baadye katika nyanja zote. Kuboresha mawasiliano baina yetu pia ni muhimu na tunawataarifu wanachama ili wafahamu zaidi kazi ya Ushirika wa Akina Mama kiujumia kama asasi, na jinsi ambayo wanachama wa Ukanda H wanaweza kushiriki.

## Shuhuda za mabadiliko

Wafungwa wa kike huko Durham walikuwa wamekosa mwelekeo na matumaini ya maisha yao ya baadaye. Askari magereza mmoja aliuliza usaidizi wa Ushirika wa Akina Mama na wanachama wakajitolea kuanzisha tawi la UAM. Waliungwa mkono na mchungaji wa gereza na hata leo, wanachama 15 hukutana kila mwezi.

Wafungwa hawa wamepata matumaini kwenye maisha yao ya baadaye kwa kujua kwamba kuna watu ambao huwaonyesha upendo na kusikiliza mahitaji yao bila kuwabagua. Tawi hili la UAM limeleta mafanikio makubwa kwa kubadilisha mtazamo wa wale wote wanaohusika. Mpango huu umepata umaarufu, mpaka UAM ikaalikwa kushiriki katika mkutano wa Nyumba ya Mabwana (House of Lords) wakati wa "Wiki ya Magereza" itakayofanyika hapo Oktoba 2020.

# Ireland Yote



**Mdhamini:** June Butler
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 7,000
**Idadi ya watu:** Millioni 6.7
**Lugha kuu:** Kiingereza, Kiairishi

Wanachama katika ukanda wetu wanawasiliana mara kwa mara na kwa tija zaidi kuliko hapo awali. Kushiriki katika kutoa shuhuda zao kumekuwa muhimu na kumezingatia faida ya kazi zao katika maisha ya wengine.

Huko Ireland Ushirika wa Akina Mama unasaidia masikini (watu binafsi na familia), wazee, wafungwa na familia zao na kila aina ya watu wenye matatizo. Pengine mafanikio yetu makubwa zaidi katika miaka ya hivi karibuni yamekuwa katika kuongeza ufahamu kuhusu unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa njia ya huduma ya kila mwaka na matukio kwa msaada wa harakati za siku 16 za kampeni. Nyingine ni kazi yetu pamoja na Women's Aid na kutoa mahitaji kwa ajili ya wanawake na watoto katika kambi za wakimbizi.

Mnamo Septemba mwaka 2020 Mkutano wa Mwaka (jina jipya la Mkutano Mkuu) utakuwa Belfast ICC katika Ireland.


Mkutano wa kila mwaka ukumbi, ICC Belfast

## Shuhuda za mabadiliko

Kikundi cha  Urafiki wa Wajane kilianzishwa mwaka wa 2001 na mmoja wa wanachama wetu ambaye aliongoza mikutano ya kila mwezi nyumbani kwake. Mwanzoni wa mwaka wa 2016 alikuwa anakaribia miaka 90 na alianza kuona mikutano imekuwa changamoto kwake. Cathedral House ilikuwa imefanyiwa ukarabati hivi karibuni, hivyo basi ilikuwa ni sahihi kuhamisha mikutano hiyo kwenye nyumba hiyo iliyofanyiwa marekebisho. Hata hivyo, hii ilihitaji usafirishaji na msaada wa vinywaji.

Wanachama katika Tawi la Templemore walialikwa kusaidia kwa mambo haya mawili na orodha ya zamu kutengenezwa. Maisie, mwanzilishi wa kundi alisema, "Mimi nilianzisha kikundi hiki ili nimsaidie rafiki yangu mjane ambaye alikuwa amefiwa hivi karibuni, ili kukabiliana na upweke wake na nilitaka kikundi hiki kiendelee kusaidia wale ambao ni wapweke". Kuhamia Cathedral House ilikuwa jambo bora, na UAM umeunga mkono kikamilifu katika kuchangia usafirishaji na vinywaji.

Wanachama wa UAM bado wanajitolea kwa ukarimu muda wao na juhudi. Kikundi kimeweza kufanya matembezi katika matamasha ya maua, chai ya mchana, sherehe ya Krismasi na ibada maalum ya kanisa. Mmoja wa wajumbe wa kikundi, Margaret alisema "Ushirika na utiwaji moyo vinazotolewa na kikundi vimekuwa msaada mkubwa katika wakati mgumu".

## Scotlandi



**Mdhamini:** Paul Hindle
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 497
**Idadi ya watu:** Millioni 5.4 **Main languages:** Kingereza, Kigaeliki

Ushirika wa Akina Mama katika ukanda wetu umeleta mafanikio makubwa kupitia mpango wa likizo uitwao 'Away From It All' (AFIA -mbali na hayo yote), kazi za gerezani na misaada ya aina mbali mbali kwa wagonjwa mahospitalini.

Dayosisi mbili zimekuwa zikihusika katika mchakato wa MULOA hadi sasa. Mwaka huu wa 2020, tunataka kuusambaza zaidi ndani ya maeneo yaliosalia ili wanachama waweze kufahamu zaidi mabadiliko wanayoweza kuleta katika jamii zao.

### Shuhuda za mabadiliko

Mwaka wa 2019 Dayosisi ya Glasgow & Galloway ilishirikiana na shirika la msaada kwa wanawake pamoja na kituo cha utafiti (Women's Aid and the Field Study Centre) kilicho mjini Millport. Ushirikiano huu ulileta mafanikio kama vile mpangilio wa safari ya siku mbili kwenda Great Cumbrae. Wanawake saba wanaolea watoto peke yao, ambao waanaathirika na vurugu za nyumbani waliweza kukaa kwa mazingira yaliyo na usalama na amani, kufanya mazoezi ya stadi za nje na kufurahia maisha pamoja na marafiki wapya. Walipata hisia ya nguvu na mtazamo chanya kwa maisha yao ya baadaye.



## Wales



**Mdhamini:** Jenny Barton
**Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama:** 5,665
**Idadi ya watu:** millioni 3.2 **Lugha kuu:** Kingereza, Kigaeliki

MULOA inaanza kutambuliwa, na wanachama wanaanza kuangalia kwa njia mpya yale wamekuwa wakitenda kwa muda mrefu,. Mafanikio yanaanza kuonekana katika maeneo mengi, ila katika dayosisi moja imewezesha matawi ambayo yalipata vitisho vya kufungwa yasifungwe. Katika tawi moja ambalo lilifungwa, waliweza kuhamisha wanachama wake kwenye dayosisi nyingine au kuwafanyia huduma zao wakiwa manyumbani kwao.

Kila dayosisi katika Mkoa wa Wales ina miradi inayoshirikisha jamii yao ambayo imesaidia watu katika hospitali au gereza, na wale wasio na makazi.

Changamoto kubwa zaidi katika ukanda wetu ni ukosefu wa usafirishaji kwa wanachama. Ninaona kipaumbele kikubwa kikiwa mafunzo ya uongozi - hii italeta mafanikio katika nyanja zote.

# Sala la kujiunga

## Jiunge na wanachama wenzako wa Ushirika wa Akina Mama kote duniani huku tukiweka familia na miradi duniani kote katika maombi yetu.

Maombi ni muhimu kwa kazi yetu kama Ushirika wa Akina Mama na kila siku, saa sita za mchana, wanachama duniani kote wanachukua muda wa kuomba. Wimbi la Maombi ni dhihirisho endelevu la kujitolea kwetu katika kuombeana sisi kwa sisi, ambalo linaendelea mwaka mzima na linashirikisha maeneo yote ambapo tumewakilishwa.

Unaweza kutumia maombi haya kila siku, kila wakati ili ujiunge na hili Wimbi la Maombi kote duniani, linaloyaombea majimbo kwa duru. Kalenda imegawanywa katika sehemu  za siku tatu wakati sisi huomba kwa ajili ya kundi la majimbo. Siku moja ya wiki kuna aya ya Biblia ambayo unaweza kutafakari juu yake na kuchukua nafasi ya kuombea masuala ya kazi ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote unayoyafikiria wakati huo.

Huku sisi tukichukua jukumu letu la kuendeleza Wimbi la Maombi, tunaweza kufanya hivyo kwa kujiamini, tukijua ya kwamba maombi yetu yana maana na nguvu. Tunajitia moyo tukijua ya kwamba duniani kote kuna wengine ambao, kwa njia hiyo hiyo wanatuombea. Na sasa kwamba *Families Worldwide* imetafsiriwa katika Kifaransa, Kihispania cha Amerika Kusini na Kiswahili ni rahisi zaidi kwetu sisi kuomba kwa ajili ya kila mmoja.

**Twamshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu nyote, tukiwataja katika maombi yetu.**

**1 Wathesalonike 1:2**

Yesu, Bwana wa uhai wetu, kwa nguvu ya neno lako na kwa njia ya matendo yako ya upendo, tuite kuwa wanafunzi wako. Tupe nguvu ya kuwa tofauti, kusimamia haki na amani na kuwa na dalili za upendo wako unaopatanisha watu wote.
Mungu wa neema, utuwezeshe sisi watumishi wako kufanya lengo lako duniani kupitia kwa  kazi ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote. Leo tunaomba kwa ajili ya : ** tazama Shajara ya Wimbi la Maombi.*

**Tunawombea wanachama wote.**
Mungu awe pamoja nao katika kila sehemu zote za maisha yao, awahimize na awaongoze, awahifadhi na awape nguvu ili waweze kufanya kazi ya kukuletea sifa na utukufu. Amina



# Utulivu

Julai 1-4 2020

### Jumatano 1
Mungu wa amani, tusamehe tunapopambana na maisha yalio na machafuko. Tusaidie kusimama, kutulia, na kufahamu kwamba wewe ni Mungu. Ruhusu roho wako atujaze roho zetu utulivu na hali iliyo shwari.

### Alhamisi 2
Mungu mwenye upendo, tunawaombea watoto wote wanaolelewa katika familia zenye vurugu na machafuko ama kutokana na mambo ya nje au yale yanayoletwa na uhusiano wenye migogoro.

### Ijumaa 3
Kwa hakika, mapumziko matakatifu ndiyo njia ya kupumzisha roho. Tunaheshimu muda wa utulivu tukiwa na Mungu. Tunaondokea kamwe ghasia za dunia. Kwa makusudi tunayakalia mbali maisha ya
ghasia. Tunafurahia muda wa utulivu.

### Jumamosi 4
Leo tunawaombea wale ambao mahitaji ya dunia hayawaruhusu kupumzika. Mungu awape amani na roho ya utulivu ili wapate mapumziko na kiburudisho maishani mwao hata wakiwa na kazi nyingi.

### Wimbi la Maombi

**1 Julai: Zambia Mashariki,** Zambia; **Mombasa,** Kenya; **Gwagwalada & Ekiti-West,** Nijeria; **Leicester,** Uingereza na **Temotu,** Visiwa vya Solomon

**2-4 Julai: Renk,** Sudan Kusini**; Cyangugu,** Rwanda; **Arochukwu/Ohafia & Ile-Oluji,** Nijeria; **St Andrews, Dunkeld & Dunblane,** Scotlandi na **Sittwe,** Myanmar

# Tumaini na Imani Julai 5-11 2020

## Jumapili 5

Basi, kuna vitu hivi viwili: Ahadi na kiapo, ambavyo haviwezi kubadilika na wala juu ya hivyo Mungu hawezi kusema uongo. Kwa hiyo sisi tuliokimbilia usalama kwake, tunapewa moyo wa kushikilia imara tumaini lililowekwa mbele yetu. Tunalo tumaini hilo kama nanga ya maisha yetu. Tumaini hilo lapenya mpaka mahali patakatifu mbinguni *Waebrania 6:18-19 (BHN)*

## Jumatatu 6

Mungu wa mbinguni, tunakushukuru kwa vile tunaishi kwa matumaini na vile tumeshikanishwa kwa upendo wako.

## Jumanne 7

Mungu wa imani, tunakusifu kwa upendo wako imara na ukweli wa Neno lako la daima, wewe ni jiwe ambalo tunajenga maisha yetu juu lake kwa matumaini na uhakika thabiti. Tusaidie kueneza tumaini lako katika kila pembe ya dunia kwa kushiriki habari njema na kuinua yote yanayoleta amani

## Jumatano 8

Leo na siku zote matumaini yetu na imani kwa Mungu iwe njia ambayo sisi tunawafikia wale ambao maisha yao yako hatarini kwa wakati huu,  ili kuwasaidia kuboresha hatima chanya. Amina

## Alhamisi 9

Chochote nitakachokabiliana nacho leo, naishi  kwa kutambua ya kwamba uhakika unatoka kwako Bwana, kwa maarifa na kujiamini kwamba wewe u pamoja nami na kwamba yote yawezekana kwa nguvu yako.

## Ijumaa 10

Tunawaombea wale wote waliokosa matumaini, wagonjwa, wale walio katika shida au hali ya hofu kwa maisha yao ya baadaye. Tunaomba waweze kupokea upendo wako wa uponyaji, pamoja na zawadi ya matumaini inayotokana na kukujua wewe.

## Jumamosi 11

Tufanye tutembee daima kwa tumaini la Kristo, tena tujiamini katika kuliamini pendo la Mungu lituunganishalo milele.

### Wimbi la Maombi

**Julai 6-8: Wad Medani,** Sudan; **Kondoa,** Tanzania; **Ikwo & Remo,** Nigeria; **Montreal, Kanada na Visiwa vya Windward,** St Lucia, Grenada, St Vincent & The Grenadines

**Julai 9-11: El Obeid,** Sudan; **Butere,** Kenya; **Nnewi,** Nijeria; **London,** Uingereza n**a Mkoa wa Marekani (USA)**

### Jumapili 12
Nitakushukuru Mungu kwa moyo wangu wote; nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu. Nitafurahi na kushangilia kwa sababu yako; nitaliimbia sifa jina lako, ewe Mungu Mkuu. *Zaburi 9:1-2*

### Jumatatu 13
Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana! Roho yangu itaimba sifa zako milele! Maneno tu hayawezi kueleza furaha kubwa ninayosikia kutokana na kukupenda wewe. Jina lako libarikiwe milele.

### Jumanne 14
Kielelezo cha juu cha ibada ni ibada ya huduma ya Kikristo bila ubinafsi. *Billy Graham, Mwinjilisti mmarekani*. Ninakujia kama nilivyo Bwana, tayari kukuabudu. Nichukue kama nilivyo na unifinyange na kunifanya kama utakavyo, ili niishi maisha yangu katika kukuabudu na kukutumikia.

### Jumatano 15
Wewe peke yako ndiwe uliye Mtakatifu, wewe ndiwe Bwana peke yako.. Mbingu na dunia zijiunge  pamoja katika kukuabudu, kwani wewe tu ndiwe unastahili kusifiwa

### Alhamisi 16
Bwana, nisaidie nitumie kila pumzi ninayopumua kukuabudu. Nikumbushe kila siku ili niachilie roho yangu ikutazame wewe, ili niweze kuruhusu lengo lako kuarifu kila ninachotenda.

### Ijumaa 17
Bwana, tusamehe kwa maana wakati mwingine tunapogubikwa na mambo yetu au matukio, upendo wetu kwako unafifia. Maisha yetu yote yawe sadaka ya ibada kwako, huku tukijitahidi kukuweka wewe mbele katika kila kitu tunachokifanya.

### Jumamosi 18
Bwana, chukua nyakati zangu na siku zangu zikiwa na shughuli nyingi au tulivu, ziwe za furaha au za huzuni, uzijaze sifa kwa ajili yako. Amina. (Sala ya kusema wakati unasubiri (ndani ya basi, katika kupanga mstari madukani, msongamano wa magari barabarani  nk) Maisha yangu ni yako, Bwana, na mimi nakupenda kwa moyo wangu wote.

### Wimbi la Maombi

**Julai 13-15: Toliara,** Bukini; **Mbale,** Uganda; **Zaria & Ndokwa,** Nijeria; **Rochester,** Uingereza na **Chhattisgarh,** India

**Julai 16-18: Lake Malawi,** Malawi; **Byumba,** Rwanda; **Jalingo,** Nijeria; **St Edmundsbury & Ipswich,** Uingereza na **Lucknow,** India

# Kujenga maisha ya uvumilivu Julai 19-25 2020

## Jumapili 19

Kumbukeni kwamba Mwenyezi-Mungu, Mungu wenu, ndiye awapaye uwezo wa kupata utajiri. Anafanya hivyo ili kuimarisha agano alilofanya na babu zenu mpaka leo *Kumbukumbu 8:18 (BHN)*

## Jumatatu 20

Uvumilivu na ustahamilivu vinakuja pale tu upewapo nafasi ya kupitia matatizo magumu. *Gever Tulley, Mwandishi na mwalimu Mmarekani*. Bwana, tafadhali tuwezeshe kusaidia wengine kukabiliana na matatizo yao ili waweze kujenga ujasiri katika maisha yao.

## Jumanne 21

Mungu ametupa zawadi ya ajabu zaidi : kutupa ufahamu kwamba anatupenda, kama tulivyo. Tunaweza kukabiliana na kitu chochote katika maisha yetu kwa sababu ya ustahamilivu ambao unakua katika nguvu ya upendo wake.

## Jumatano 22

Bwana utupendaye, tunaomba kwamba watu, familia na jamii ziweze kubadilishwa ili zipate ujasiri na mafanikio kupitia kazi ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote.

## Alhamisi 23

Bwana, tunatoa shukrani kwamba ni wewe tu ambaye hubadiliki katika ulimwengu unaobadilika kila wakati. Tafadhali kuwa nasi katika hali tuliyo nayo leo na kutupa ustahamilivu tunaohitaji ili kukabiliana na vikwazo, ili tuweze kukamilisha mambo uliyoweka mbele yetu.

## Ijumaa 24

Mungu mtoaji, tunaomba leo utupe uwezo wa kujenga ustahamilivu na hali ya kujitosheleza kwa ajili ya wale ambao wamepoteza nguvu kutokana na mahitaji ya maisha na ustahamilivu wa kila siku.

## Jumamosi 25

Bwana wetu, asante kwa vile wewe ni mahali patakatifu na malazi, chochote kinachoendelea katika maisha yangu. Nipe nguvu za Roho wako Mtakatifu ili niweze kujitokeza katika ulimwengu nikijiamini, nikiwa nimejazwa na upendo wako unaokomboa watu. Amina.

## Wimbi la Maombi

**Julai 20-22: Gitega,** Burundi; **Murang'a South na Mbeere,** Kenya; **Enugu North,** Nijeria; **Polynesia,** Tonga na **Jaffna,** India

**Julai 23-25: George,** Afrika Kusini; **Bungoma,** Kenya; **Tanganyika Magharibi,** Tanzania; **Ideato,** Nijeria; **Sodor & Man,** Isle of Man na **Toronto,** Kanada

### Jumapili 26
Yesu akamjibu, "Imeandikwa: 'Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno asemalo Mungu' *Mathayo 4:4 (BHN)*

### Jumatatu 27
Bwana wa upendo, tunaposoma Neno lako leo tupe akili zinazohoji na moyo mkunjufu. Tutayarishe kukabiliana na changamoto ya kukumbatia ndoto za Neno hilo. Katika kila hali ya maisha yetu Biblia iwe taa kwa miguu yetu na mwangaza wa njia yetu.

### Jumanne 28
Tunapaswa kuruhusu Neno la Mungu likabiliane na sisi, livuruge usalama wetu lidhoofishe kuridhika kwetu na kuipindua mpagilio wa mawazo na tabia zetu.. *John Stott, 1921-2011*, Kuhani na mwana-theolojia wa kanisa la Anglikana

### Jumatano 29
Bwana Mungu, tunakushukuru kwa njia mbalimbali ambazo sisi kama Ushirika wa Akina Mama tunayatumia mafunzo ya Biblia kwa kutambua uongozi wako katika mipango yetu ya kanisa na jamii. Tunaomba uendelee kufungua ukweli uliomo katika Neno lako huku tukitafakari kwa uwazi.

### Alhamisi 30
Bwana, tunawaombea wale ambao husambaza Neno lako katika maeneo ambayo ni hatari kusambaza Biblia. Huku wakitoa kwa ajili ya wale ambao wanatamani maandikopo, Roho wako Mtakatifu awaongoze na kuwalinda.

### Ijumaa 31
Tunamshukuru Mungu kwa nguvu ya Neno lake, ambalo ni hai na linafanya kazi katika maisha yetu; ambalo linatujaza nguvu zake na mwanga wake. Tunamshukuru Mungu, kwa ajili ya Yesu, Neno hai. Aishi milele kati yetu, akituunganisha pamoja; akigusa maisha yetu kwa neema yake ya kudumu na ukweli

## AGOSTI
### Jumamosi 1
Chukua muda leo kutafakari juu ya sehemu ya Maandiko. Muulize Mungu akuonyeshe ukweli mpya na kukupa muongozo wakati unaposoma na kuomba.

### Wimbi la Maombi
**Julai 27-29: Northern Zambia,** Zambia; **Mpwapwa,** Tanzania; **Gusau & Osun,** Nijeria; **Sydney,** Australia na **Rayalaseema,** India

**Julai 30 -Agosti 1: Boga,** JD Kongo; **Manicaland,** Zimbabwe; **Tanga,** Tanzania; **Ogoni** Nijeria; **Carlisle**

## Kupumzika kwa mwili na roho Agosti 2-8 2020

### Jumapili 2
Mwenyezi-Mungu ni mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Hunipumzisha kwenye malisho mabichi;huniongoza kando ya maji matulivu. . Kweli wema wako na fadhili zako zitakuwa pamoja nami, siku zote za maisha yangu;nami nitakaa nyumbani mwa Mwenyezi-Mungu milele. *Zaburi 23:1-2, 6*

### Jumatatu 3
Tunakushukuru, Bwana, kwa ajili ya mapumziko na utulivu, kwa nafasi ya kujitoa katika mahangaiko ya maisha. Tunaomba ya kwamba leo, hata tukiwa na kazi nyingi, utatupatia kiburudisho cha kiroho katika kukuza imani katika nafsi zetu.

### Jumanne 4
Niliona kwamba Mungu ndiye amani yetu ya kweli... Anatulinda pale ambapo hatuwezi kupata mapumziko... Kwa hivyo Mungu ni mwamba wetu wa hakika, na yeye atakuwa furaha yetu kamili, na kutufanya kama yeye tusibadilike, tufikapo mbinguni. *Julian wa Norwich*

### Jumatano 5
Mungu wa huruma, pumua upendo ndani na kati yetu.. Kutoka muda mmoja hadi mwingine, unatushikilia katika kiganja cha mkono wako. Kuwa nasi leo na uwe na wale wote ambao wanahitaji kiburudisho na upendo wako usio na mwisho.

### Alhamisi 6
Tunawaombea wale ambao wana hofu na kulemewa na mizigo, wale ambao wamechoshwa na shughuli za maisha. Wapate matumaini na nguvu mpya kwa neema ya Mungu, tena waweze kupata mapumziko ndani ya upendo wake.

### Ijumaa 7
Bwana utupendaye, tunaomba kwa ajili ya wale wote wanaojitolea; ili kutunza majirani zao bila kujali, na kuangaza mwanga wa Kristo katika dunia hii. Naomba wao pia wapate mapumziko, huku wakijitenga mbali na mahitaji ya dunia ili wapate kutakaswa mbele ya Mungu.

### Jumamosi 8
Bwana leo ningependa tu kukaa kimya na kutulia katika uwepo wako, nisikilize pumzi ya Roho wako na kufahamu upendo wako wa hali ya juu kwangu, mimi mtoto wako.

### Wimbi la Maombi

**Agosti 3-5: Juba,** Sudan Kusini; **Kitale,** Kenya; **Minna & Lagos,** Nijeria; **Moray, Ross & Caithness,** Scotlandi, na **Madurai-Ramnad,** India

**Agosti 6-8: Malawi Kaskazini,** Malawi; **Eldoret,** Kenya; **Ngbo & Akure,** Nijeria; **North West Australia,** Australia,na **Aipo Rongo,** PNG

## Jumapili 9 Siku ya Mary Sumner

Tunawatakieni neema na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. Ndugu, tunapaswa kumshukuru Mungu daima kwa ajili yenu. Inafaa kwetu kufanya hivyo kwani imani yenu inakua sana na kupendana kwenu kunaongezeka sana. *2 Wathesalonike 1:2-3 (BHN)*

## Jumatatu 10

Baba wa upendo, tunajiunga na familia zetu duniani kote, kwa sauti moja, ili tulitukuze jina lako. Tuwe na umoja katika kusudi; tukiongozwa na imani kwa wakati wa sasa na kwa matarajio yetu ya baadaye. Amina

## Jumanne 11

Ushirika wa Akina Mama umenisaidia kumkaribia Mungu kwa sababu kila kitu ninachofanya kinahusiana kabisa na maombi na imani. Jambo hili linahusisha kushiriki katika familia kubwa zaidi inayofanya kazi na kuomba pamoja.
*Mwanachama wa Ushirika wa Akina Mama*

## Jumatano 12

Nina furaha iliyoje kuwa sehemu ya familia inayoenea duniani kote, tukishiriki pamoja katika lengo letu la kuunga mkono maisha ya familia. Huku tukishiriki katika tofauti za utamaduni katika familia yetu ya Ushirika wa Akina Mama, tunaomba Mungu atuongoze ili tuelewe maisha ya wengine.

## Alhamisi 13

Bwana wa upendo, tunatoa shukrani kwa nafasi ya kuhudumia familia ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote. Tunaomba familia yetu iwe na umoja, tukitumainia na kuendelea kuwafikia watu duniani kote, sisi tukiwa kama mikono yako.

## Ijumaa 14

Upendo wetu kwa Mungu ndiyo unashikilia familia ya Ushirika wa Akina Mama pamoja. Bwana, tusaidie kusaidiana sisi kama familia na kuwafadhili wale tunaowahudumia.

## Jumamosi 15

Bwana, tunakushukuru kwa upendo na urafiki ambao unatuzingira tunapoishi kwa imani yetu katika familia ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote.

### Wimbi la Maombi

**Agosti10-12: Niassa,** Msumbiji; **Masindi Kitara,** Uganda; **Langtang & Esan,** Nijeria; **North Queensland,** Australia na **Kolhapur,** India

**Agosti 13-15: Natal,** Afrika Kusini; **Kajiado,** Kenya; **Okigwe & Western Izon,** Nijeria; **Nova Scotia & Prince Edward Island,** Kanada, na **Toungoo,** Myanmar

## Jumapili 16

Nakusifu maana nimefanywa kwa namna ya ajabu, matendo yako ni ya ajabu; wewe wanijua kabisakabisa. Umbo langu halikufichika kwako nilipotungwa kwa siri na ustadi ndani ya dunia. Wewe uliniona hata kabla sijazaliwa, uliandika kila kitu kitabuni mwako siku zangu zote ulizipanga, hata kabla ya kuweko ile ya kwanza. *Zaburi 139:14, 16*

## Jumatatu 17

Bwana, naomba kwamba niweze kuona maajabu ya kila kitu katika jicho la mtoto na kufahamu hatia na msisimko unaotokana na mawazo.

## Jumanne 18

Kama vile mtoto hukua hadi kufikia ujana, naomba kwamba roho ya matumaini iwe ndani yangu. Tena nipate uwezo usio na mwisho katika maisha. Asante Bwana, kwa matarajio na uwezekano, mambo ambayo yanaambatana na msimu huu wa maisha.

## Jumatano 19

Katika msimu wa kiangazi, tunapata nguvu na kuzaa matunda ya Roho - upendo, furaha, amani, subira, wema, fadhili, uaminifu, upole, na kujizuia. Bwana, naomba kwamba hiyo nuru iendelee kung'aa katika mioyo yetu.

## Alhamisi 20

Usihukumu kila siku kwa mavuno unayopata lakini kwa mbegu ambazo umepanda. *Robert Louis Stevenson*. Tunasherehekea kupanda na kuvuna mbegu zetu. Tunatoa shukrani kwa zawadi nyingi ambazo sisi sote tunaweza kuchangia jamii.

## Ijumaa 21

Majira ya baridi ni wakati wa kupumzika na kutafakari. Turekebishe mioyo yetu, Bwana ili tukuone wewe wazi zaidi, tukupende zaidi, tena tukukaribie zaidi siku hadi siku. Asante kwa zawadi ya kila msimu, na kwa kuufanya kila msimu uwe na uzuri wake kwa wakati wake.

## Jumamosi 22

Kila kitu kina majira yake, kila jambo duniani lina wakati wake: *Mhubiri 3: 1.* Bwana utupendaye, tunaweka mikono yetu katika mikono yako ili tuweze kuvuka kila msimu, na tunaamini katika upendo na uaminifu wako, ukiwa kiongozi wetu kwa kila badiliko la msimu.

### Wimbi la Maombi

**Agosti 17-19: Kasai,** JD Kongo; **Shyira,** Rwanda; **Ijumu & Egba Magharibi,** Nijeria; **Liverpool,** Uingereza na **Sambalpur,** India

**Agosti 20-22: Zimbabwe ya Kati,** Zimbabwe; **Lango,** Uganda; **Kebbi,** Nigeria; **Tamale,** Ghana; **Sheffield,** Uingereza, na **Guadalcanal,** Visiwa vya Solomon

### Jumapili 23
Nia yetu ni kufanya vyema, si mbele ya Bwana tu, lakini pia mbele ya watu..
*2 Wakorintho 8:21 (BHN)*

### Jumatatu 24
Bwana, kuna mambo mengi tunayosikia katika habari ambayo yanaonekana kuwa na makosa. Tusaidie kusema bila kuficha wakati tunapoweza, kuweka mfano na kuwa na ujasiri mbele ya upinzani. Tusaidie kutegemea njia zako ili tusiyumbishwe na mitazamo ya dunia

### Jumanne 25
Maadili ni kujua tofauti baina ya kile ambacho una haki ya kufanya na jambo ambalo ni haki kulifanya. *Potter Stewart, Jaji Mmarekani, 1915-1985*. Mungu wa haki na huruma, tunaomba utupe daima nguvu ya kufuata njia yako ya haki.

### Jumatano 26
Tunaomba tupate hekima na ufahamu wa kuona njia tunayofaa kufuata katika majadiliano wakati tunajikuta katika mkanganyiko wa kimaadili. Roho Mtakatifu atuongoze kufanya maamuzi kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu.

### Alhamisi 27
Mungu mwenye haki, tunaombea dunia yako ambapo watu wengi wapo kwa uhitaji. Tusaidie kufanya maamuzi sahihi hata kama yanaweza kutugharimu zaidi au kuchukua muda mrefu zaidi ya njia zingine zisizo za kimaadili.

### Ijumaa 28
Tunawaombea wale wote wanaoteseka kutokana na biashara, shughuli na maisha, yasiofuata maadili. Tunawaombea watoto wanofanya kazi nzito kwa muda mrefu zaidi, katika hali mbaya. Tunawaombea wasichana na wanawake waliopo katika biashara ya ngono na zingine zisizo halali. Tunawaombea wazazi ambao, katika kujaribu kujisaidia wenyewe na familia zao, wanakuwa wahanga wa utumwa wa mamboleo.

### Jumamosi 29
Bwana, tusaidie kusikiliza na kuelewa wale walio na maoni tofauti juu ya masuala ya kimaadili. Tunakubali kwamba mara nyingi hakuna jibu sahihi; Utuongoze ili tuchague njia bora ya kuendelea mbele pale ambapo njia zote zina makosa.

### Wimbi la Maombi
**Agosti 24-26: Saldanha Bay,** Africa Kusini; **Karamoja,** Uganda**; Udi & Etsako,** Nijeria; **Wellington,** Nyuzilandi na **Yangon,** Myanmar

**Agosti 27-29: Matabeleland,** Zimbabwe; **Mount Kenya Central,** Kenya; **Niger Magharibi,** Nijeria, **Wangaratta,** Australia; **Clogher,** Ireland Yote, na **Hpa-An, Myanmar**

# Kurasa Mpya Agosti 30-Septemba 5 2020

## Jumapili 30

Mwenyezi-Mungu atakukinga na baya lolote; atayalinda salama maisha yako.
*Zaburi 121:7-8 (BHN)*

## Jumatatu 31

Bwana utupendaye, tunawakabidhi kwa utunzaji wako watoto wote na wanafunzi wanaoingia kwenye njia mpya za maisha yao wakati huu.

## SEPTEMBA

## Jumanne 1

Tunaomba kwa ajili ya wote wanaofanya kazi katika shule zetu na vyuo, ili wabarikiwe na shauku na nguvu, hekima na busara wakiwa mbele ya utukufu na changamoto za kila mwanzo mpya katika mwaka huu wa kitaaluma.

## Jumatano 2

Bwana wa imani, wakati tunaanza kurasa zisisimuazo za maisha yetu mapya, tungependa kwamba ushirikiano wetu na wewe uwe na mizizi ya kweli na kuendelea kukua kupitia nafasi zote mpya tunazozipata.

## Alhamisi 3

Bwana wa imani, wakati tunapata changamoto mbele yetu katika mwanzo wa kurasa mpya za maisha yetu, tunaomba utuondolee hofu na giza, na kutukaribisha kwa upendo wako, huku tukiweka mikono yetu katika mikono yako – na kukuamini wewe katika fursa zote mpya tunazozipata.

## Ijumaa 4

Bwana wa imani, kila tunapoanza kurasa mpya, tupe nguvu ya kubeba furaha na huzuni zetu, nguvu ya kuangalia nje na kuunga mkono uadilifu, huku tukikabiliana na udhalimu, nguvu ya kupambanua na kusikiliza sauti yako tulivu na dogo; tukiendelea kuwa na tumaini kwenye upendo wako usio na mwisho.

## Jumamosi 5

Bwana, tunataka utuvuruge, ili tuthubutu kwa ujasiri zaidi, ili tuwe na moyo wa kujaribu wakati wa dhoruba huku ukituonyesha miujiza yako; na ambapo kama hatutaweza kuona nchi kavu, tupate kuona nyota. *Sir Francis Drake, Elizabethan* Admiral

### Wimbi la Maombi

**Agosti 31-2 Septemba: Harare,** Zimbabwe; **Machakos,** Kenya; **Ogori-Magongo & Ekiti,** Nijeria; **Southwark,** Uingereza na **Phulbani,** India

**Septemba 3-5: Khartoum,** Sudan; **Dar es Salaam,** Tanzania; **Bari & Ilesa,** Nijeria; **Gloucester,** Uingereza, na **Dugapur,** India

# Kujifunza na Kushirikiana Septemba 6-12 2020

## Jumapili 6

Basi, wewe mwanangu, uwe na nguvu katika neema tunayopata katika kuungana na Kristo Yesu. Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine. *2 Timoteo 2: 1-2 (BHN)*

## Jumatatu 7

Baba, tunaomba tuweze kujifunza kusimama na kusikiliza Neno lako, kusikia sauti yako na kufuata njia yako katika maisha yetu. Tusaidie kujifunza kutokana na mfano wako, mambo ambayo ni muhimu zaidi katika maisha.

## Jumanne 8

Bwana wa upendo, tuwezeshe daima kupata muda wa kusikilizana na kujifunza kati yetu. Ujuzi na hekima viendelee kukuwa kati yetu kwetu, huku tukitafakari juu ya masuala mapya.

## Jumatano 9

Ee Mungu wa ukarimu kila mmoja ameendeleza vipawa ambavyo wewe umetupatia. Tunataka daima tuwe tayari kushiriki zawadi hizi katika ulimwengu ili tusaidie wengi walio karibu nasi kufurahia maisha yaliyo na mafanikio kamili.

## Alhamisi 10

Kujifunza ndiyo jambo pekee ambalo akili haiwezi kamilisha. Haihofi wala haiwezi jutia. *Leonardo da Vinci, 1452-1519*. Kujifunza hakuna mwisho, ni safari inayoendelea. Tunaomba daima tuwe na hamu ya kujifunza na kutoa ujuzi wetu kwa wengine.

## Ijumaa 11

Bwana, tunaomba usaidie wale wote ambao elimu ni changamoto kwao kwa sababu ya mahitaji yao maalum. Wapate walimu hodari wenye moyo wa kuwajali, ambao wanaweza kufungua uwezo wao wa kuelewa na kuwaonyesha furaha ya kujifunza.

## Jumamosi 12

Shukrani kwa ajili ya mafanikio ya Mpango wa Kusoma na Kuandika na Elimu ya Kifedha unaotekelezwa na UAM katika nchi mbalimbali. Tunawaombea wale ambao maisha yao yanabadilishwa, wawezeshaji wetu, na wale wanaoendelea kusaidia kazi hii muhimu.

## Wimbi la Maombi

**Septemba 7-9: Pacong,** Sudan Kusini; **Nyanza Kusini,** Kenya; **Kutigi & Ijesha Kaskazini,** Nijeria; **Bristol,** Uingereza na **Karnataka Kati,** India

**Septemba 10-12: Pretoria,** Afrika Kusini; **Mbale Kakazini,** Uganda; **Oke-Osun,** Nijeria; **Exeter,** Uingereza na **Barbados**

# Kuzaa Matunda Septemba 13-19 2020

## Jumapili 13

Kaeni ndani yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile tawi haliwezi peke yake kuzaa matunda lisipobaki katika mzabibu, hali kadhalika nanyi hamuwezi kuzaa matunda msipokaa ndani yangu. "Mimi ni mzabibu, nanyi ni matawi. Akaaye ndani yangu, nami nikiwa ndani yake, huyo huzaa matunda mengi, maana bila mimi hamuwezi kufanya chochote. *Yohana 15:4-5*

## Jumatatu 14

Kiasi cha muda tunaotumia pamoja na Yesu - tukitafakari neno lake na utukufu wake, kwa kutafuta radhi yake - kinaimarisha mafanikio yetu katika ufalme.
*Dr Charles Stanley, Mchungaji Mmarekani.*

## Jumanne 15

Kristo aishi katika mioyo yetu kwa imani, tustawi katika upendo wake, na maisha yetu yaonyeshe matunda ya Roho wake Mtakatifu leo na kila siku.

## Jumatano 16

Naomba ya kwamba Kristo akiwa anaishi ndani yangu, nami ndani yake, nitakuwa tawi lizaalo matunda mengi.

## Alhamisi 17

Bwana, tusaidie kuzaa matunda katika kazi zetu kwa ajili ya UAM. Tuendelee kuanzisha mipango ambayo huwaletea matumaini wanyonge, wale waliovunjika moyo, na wale waliokata tamaa.

## Ijumaa 18

Roho Mtakatifu, pumua maisha ndani yangu leo, ili nizae mbegu za upendo, amani na huruma ambazo umepanda ndani yangu. Unilee mimi katika ukomavu na uzaaji kwa ajili ya wote karibu nami.

## Jumamosi 19

Asante Bwana kwamba mbegu zilizopandwa na Mary Sumner zimekua na kustawi duniani kote. Tunaomba ili nguvu za Roho wako Mtakatifu ziendelee kuleta kukomaa kwa mbegu ambazo zinapandwa.

## Wimbi la Maombi

**Septemba 14-16: Mthatha,** Afrika Kusini; **Namirembe,** Uganda; **Pankshin & Sabongidda-Ora,** Nijeria; **Dublin & Glendalough,** Ireland Yote na **Central Solomons** Visiwa vya Solomon

**Septemba 17-19: Buye,** Burundi; **Sebei,** Uganda; **Abakaliki & Ekiti-Oke,** Nijeria; **Southwell & Nottingham,** Uingereza na **Belize**

# Amani na usalama Septemba 20-26 2020

## Jumapili 6
Nalala na kupata usingizi kwa amani; ee Mwenyezi-Mungu, wewe peke yako waniweka salama. *Zaburi 4:8*

## Jumatatu 21
Mungu wa amani, tunaomba ulete matumaini kwa watu wako ambao wanaishi katika nchi zilizo na migogoro. Wapate usalama wakiwa ndani ya mazingira ambayo sisi hatuwezi kufikiria.

## Jumanne 22
Naamini kwamba Mungu, kwa njia ya Roho wake, hutupa upendo, furaha na amani bila kujali kinachoendelea katika maisha yetu. Kama Wakristo, hatupaswi kutarajia furaha yetu ituridhishe daima, lakini badala yake, tutambue furaha kama usalama wa ndani – kuwa na usalama katika maisha yetu na Kristo. *Jill Briscoe, Mwandishi*

## Jumatano 23
Tunawaombea wanachama wetu duniani kote walio katika hali ya vita, na wale wanaoishi baada ya vita. Na wafungue njia ili kuleta amani na maridhiano kwa njia ya msaada kwa vitendo, hisia na kiroho kwa ajili ya waathirika wa unyanyasaji na wale wakimbizi wanaokimbia vita vya wenyewe kwa wenyewe.

## Alhamisi 24
Tunawaombea wale wanaotetea masuala ya amani na usalama mbele ya wanasiasa na watoa maamuzi katika ngazi zote. Na wapate ushawishi chanya juu ya wale ambao wanatangamana nao.

## Ijumaa 25
Tunawaombea wanachama wetu duniani kote ambao huingilia kwa upole, kupitia ukarimu na upendo, ili kupatanisha familia na jamii na kurekebisha uhusiano kati yao. Tunashukuru kwa ajili ya huduma ya upatanisho, inayopatikana kwa njia salama ambayo hutolewa bila kuwahukumu wahusika.

## Jumamosi 26
Bwana Yesu, wewe uliwasalimu wanafunzi wako kwa maneno, 'Amani iwe nanyi'. Tunataka pia, kusikia maneno yako na kuijua amani yako katika mioyo yetu leo na daima.

### Wimbi la Maombi

**Septemba 21-23: Rumbek,** Sudan Kusini; **Soroti,** Uganda; **Aba Ngwa North & Oyo,** Nijeria; **Peterborough,** Uingereza na **North Eastern Caribbean & Aruba**

**Septemba 24-26: Makamba,** Burundi; **North Karamoja,** Uganda; **Lokoja & Sapele;** Nijeria; **Truro,** Uingereza na **Tirunelveli,** India

# Heshima kwa wazee Septemba 27-Oktoba 3 2020

## Jumapili 27
Mimi ni yuleyule hata katika uzee wenu; hata katika uzee wenu mimi nitawabeba. Nilifanya hivyo kwanza, nitafanya hivyo tena. Nitawabeba nyinyi na kuwaokoa. *Isaya 46:4*

## Jumatatu 28
Bwana, tunaomba uwe nguvu na tegemeo la wote ambao wanahudumia watu wazee katika familia zao na jamii. Wape uvumilivu na hekima ya kusikiliza na kuelewa mahitaji halisi ya watu wanaohudumia.

## Jumanne 29
Leo tunaomba tupate mahusiano ya kweli kati ya vizazi mbalimbali. Tunaomba wawe na heshima kubwa huku kila mmoja wao akijifunza kuhusu changamoto zinazowakabili vijana wa leo, na mabadiliko ambayo wazee wameshapitia.

## Jumatano 30
Tunajua, Bwana kwamba huwezi kututupilia mbali katika muda wa uzee, tunajua kwamba huwezi kutuacha wakati nguvu zetu zimetumika (Zaburi 71: 9). Asante kwa uaminifu wako kwetu katika maisha yetu.

## OKTOBA
## Alhamisi 1
Tunawaombea wazee ambao kutokana na matatizo ya kimwili au afya ya kiakili, wana ugumu wa mawasiliano na shughuli za kila siku. Wapate msaada wanaohitaji kwa hadhi na heshima.

## Ijumaa 2
Darasa bora kabisa duniani lipo chini ya ulinzi wa mtu mzee. *Andy Rooney, mwandishi wa habari*. Bwana, tunakuomba utufundishe kuchukua muda wa kushiriki katika mazungumzo, kusikiliza na kuheshimu maoni ya wakubwa wetu tunapokutana nao.

## Jumamosi 3
Toa shukrani kwa ajili ya wazee unaowajua, au wale uliopata kuwajua, ambao wamejitolea sana kwa ajili ya familia zao, makanisa yao na Ushirika wa Akina Mama. Ombeni ili tupate kufuata mfano wao wa kupenda kazi ya uaminifu.

### Wimbi la Maombi

**Septemba 28-30: Katanga,** JD Kongo; **Rwenzori,** Uganda; **Mbaise & Egba,** Nijeria; na **Tiruchirappalli Thanjavur,** India

**Oktoba 1-3: Nzara,** Sudan Kusini; **North Kigezi,** Uganda; **Kivu,** Rwanda; **Damataru,** Nijeria; **Auckland,** Nyuzilandi na, **Vanuatu na New Caledonia,** Vanuatu

# Saidianeni kubeba mizigo yenu Oktoba 4-10 2020

## Jumapili 4
Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatimiza sheria ya Kristo. *Wagalatia 6:2 (BHN)*

## Jumatatu 5
Kuna giza sana katika ulimwengu wetu, Bwana; ni vigumu kujua jinsi ya kuleta mabadiliko. Tusaidie kuona ulimwengu kama wewe unavyouona ili tufahamu mahitaji ya wale walio karibu nasi, na jinsi tunavyoweza kuwa mikono na miguu yako duniani.

## Jumanne 6
Lazima tutegemeane, tutulizane, tupeane msaada na kushauriana, kwani kipimo cha maadili ya kila mtu yanadhihirika katika wakati wa matatizo - matatizo ambayo hayadhoofishi mtu bali yanaonyesha yeye ni nani. *Thomas Kempis, 1380-1471*

## Jumatano 7
Ombea leo mtu unayemfahamu, ambaye anasumbuliwa na matatizo katika maisha yake ya kila siku. Muombee ili mzigo wake uweze kuondolewa, ili aweze kupata na kukubali msaada anaouhitaji.

## Alhamisi 8
Waombee leo familia na jamaa zako na hasa mtu yeyote ambaye ni mgonjwa au mwenye huzuni kwa sababu yoyote. Tafakari juu ya msaada unaoweza kumpa au kumtafutia.

## Ijumaa 9
Tunawaombea wote ambao husikiliza wale waliozidiwa na wasiwasi na dhiki. Wawe na hekima na ufahamu kutoka kwa Mungu, ili wajue jinsi ya kuwasaidia, wakati wa kutoa maoni yao, na kile watakachosema ili waweze kusaidia kwa njia ya maana.

## Jumamosi 10
Fikiria ngamia ambaye hakuweza kupitia mlango mwembamba kwa sababu ya mzigo mzito aliokuwa amebeba. Tafakari juu ya ziada yoyote ya “mizigo” unaweza kuwa unabeba, na uombe ili uweze kuitua. Tupa mashaka yako yote kwa Mungu. Yeye atayabeba ili uwe huru.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 5-7: Mbhashe,** Afrika Kusini; **Kitgum,** Uganda; **Ukwa & Ilesa South-West** Nijeria; **Tasmania,** Australia, na **Melanesia ya Kati,** Visiwa vya Solomon

**Oktoba 8-10 Ethiopia; Zanzibar,** Tanzania; **Awgu/Aninri,** Nijeria; **Freetown,** Sierra Leone**; Monmouth,** Wales na **Malaita** Visiwa vya Solomon

## Jumapili 11

Mwenyezi-Mungu alipoturekebisha na kuturudisha Sayuni, tulikuwa kama watu wanaoota ndoto! Hapo tuliangua kicheko; tulishangilia kwa furaha. Nao watu wa mataifa mengine walisema: "Mwenyezi-Mungu amewatendea mambo makubwa!" *Zaburi 126:1-2*

## Jumatatu 12

Baba wa mbinguni, tunawakumbuka wafungwa waliotengwa na familia zao, hasa wale ambao hawatembelewi na mtu yeyote. Tunaomba kwa ajili ya kazi ya wana-chama wetu ambao hutumika kwa njia mbalimbali katika mfumo wa gerezani.

## Jumanne 13

Leo ni siku ya kimataifa ya Elimu katika Gereza, kwa hiyo tunawaombea wote ambao hufanya kazi katika ukarabati, wale wanaofundisha ujuzi ili kuwawezesha wafungwa kupata nafasi katika jamii wanapotoka gerezani, ili wasivunje sheria tena.

## Jumatano 14

Tunaomba baraka yako Bwana, kwa kila mtu ambaye anafanya kazi katika huduma ya gerezani. Wape nguvu ya kusimamia haki wakiwa na huruma, ili kuhakikisha ustawi na makazi mapya ya wahalifu. Wapate msaada wanaohitaji ili wafanikiwe katika majukumu yao mbalimbali.

## Alhamisi 15

Bwana wa upendo, tunawaombea wote walio gerezani kwa ajili ya imani yao. Tunaomba wawe daima na ufahamu wa uwepo wako na wapate ujasiri kwa kujua kwamba watu duniani kote wanawaombea.

## Ijumaa 16

Sikiliza, Bwana, maombi ya wale ambao wameshikwa mateka kwa udhalimu. Sala inayosemwa kupitia meno yaliyokazwa kwa ajili ya hofu, sala inayoelea kwa ujasiri katika wimbi la kukata tamaa, sala ambazo ni uzi mwembamba wa matumaini.

## Jumamosi 17

Baba uliye mbinguni, leta faraja kwa familia za wafungwa, ambao pia wanatumikia adhabu kwa njia tofauti. Wape ujasiri na tegemeo kwa wakati huu na matumaini ya mabadiliko katika siku zijazo.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 12-14: Ezo** Sudan Kusini; **Thika,** Kenya; **Jos & Akoko,** Nijeria; **Uropa** na **União de Mulheres Episcopais Anglicanas do Brasil (UMEAB),** Brazil

**Oktoba 15-17: Terekeka,** Sudan Kusini; **Nairobi,** Kenya; **Maiduguri & Osun North,** Nijeria; **Edinburgh,** Scotlandi na **Calcutta,** India

## Jumapili 18
Usimnyime mtu anayehitaji msaada, ikiwa unao uwezo wa kufanya hivyo. Usimwambie jirani yako aende zake hadi kesho, hali wewe waweza kumpa anachohitaji leo. *Methali 3:27-28*

## Jumatatu 19
Bwana, fungua macho yetu ili tuone mapungufu yanayotuzunguka, ambayo pengine hayaonekani wazi kwa sababu ya vingi tulivyonavyo. Tupe neema ya kufikia wengine kwa huruma na kwa njia ya vitendo, kwa gharama yoyote kwetu wenyewe.

## Jumanne 20
Baba wa mbinguni, tunaomba kwa ajili ya watoto ambao wana utajiri wa mali lakini wanakosa upendo na kujaliwa kwa makini. Uwaletee katika maisha yao watu watakaotumia wakati wao ili watoto hawa washamiri kihisia na wapate furaha.

## Jumatano 21
Tunaomba leo kwa ajili ya jamii duniani kote ambazo zinashiriki katika mipango ya kanisa na jamii kwa kukabiliana na mapungufu, kwa kutumia vizuri rasilimali walizo nazo tayari. Tunamshukuru Mungu kwa wanachama wetu ambao wanashiriki katika kazi hii.

## Alhamisi 22
Mungu mwenye haki, tunaomba dhidi ya serikali ambazo, kwa udhalimu, zinanyima watu uhuru wao kwa sababu ya imani yao ya kisiasa au ya kidini.

## Ijumaa 23
Bwana wa upendo, tunakushukuru kwa ajili ya utoaji wa mahitaji binafsi yanayotolewa na Ushirika wa Akina Mama duniani kote. Tunaomba kwamba kila zawadi itakayotolewa ya vifaa vya kutumika maishani itampamba mpokeaji wake kwa heshima na kukubalika kama ishara ya neema ya Mungu.

## Jumamosi 24
Tumekosa kufahamu asili ya umaskini, na kudhani kwamba ni umaskini wa kiuchumi. Hapana, umaskini ni ule wa roho, kunyimwa upendo wa Mungu, ulio wa kuburudisha na amani. *Thomas R. Kelly, 1893-1941*

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 19-21: High Veld,** Afrika Kusini; **Nambale,** Kenya; **Niger-Delta,** Nijeria; **Guinea; Blackburn,** Uingereza na **Bhopal,** India

**Oktoba 22-24: Kimberley and Kuruman,** Afrika Kusini; **Kitui, Kenya; Kano & Kwara,** Nijeria; **Armidale,** Australia, **Myitkyina,** Myanmar

# Kusherehekea watu wa Mungu Oktoba 25-31 2020

## Jumapili 25
Kabla ya kuumba ulimwengu, Mungu alituteua tuwe wake katika kuungana na Kristo ili tuwe watakatifu na bila hitilafu mbele yake. Kwa sababu ya upendo wake, Mungu alikuwa ameazimia tangu zamani kutuleta kwake kama watoto wake kwa njia ya Yesu Kristo. Ndivyo alivyopenda na kunuia. Basi, tumsifu Mungu kwa sababu ya neema yake tukufu ambayo ametujalia katika Mwanae mpenzi!.*Waefeso 1:4-6 (NLT)*

## Jumatatu 26
Bwana wa historia na milele, tunakusifu kwa ajili ya watu wako katika nyakati zote - baadhi ya majina maarufu, wengine wanaojulikana na wachache tu - ambao maisha yao yaling'ara kama mwanga kwa wale walio gizani, na kuwaongoza katika ufalme wa Mungu.

## Jumanne 27
Tunashukuru leo kwa ajili ya watu wale ambao walituongoza kwenye njia ya Kristo wakitumia maneno na matendo yao.

## Jumatano 28
Ukisoma historia utaona kuwa Wakristo ambao walifanya mengi zaidi kwa ajili ya dunia ya sasa walikuwa hasa wale ambao waliwaza mengi kwa dunia ijayo.
*CS Lewis, 1898-1963, Mwandishi Mkristo*

## Alhamisi 29
Asante, Bwana, kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama ambao hukuhudumia bila kuchoka kwa njia ambazo hazionekani na wengi. Naomba wahakikishiwe upendo wa Mungu huku wakiangaza utukufu wake kupitia maisha yao.

## Ijumaa 30
Tunakumbuka leo kwa shukrani shahidi isiovunjika ya Ukristo, karne hadi karne, Ukristo uliosimama imara hata nyakati za shida na mateso.

## Jumamosi 31
Mungu wa kicheko na furaha, tunakugeukia wewe wakati wa All Hallows Eve, kama vile mababu zetu walifanya tangu zamani za kale. Angaza njia ya wale wanoadhimisha usiku wa leo na kuwafunga katika upendo wako ili wajue neema yako, pamoja na watakatifu wote wa mbinguni.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 26-28: Malakal,** Sudan Kusini; **All Saints Cathedral,** Kenya; **Kontagora & Osun North East,** Nijeria; **Glasgow & Galloway,** Scotlandi na **Pune,** India

**Oktoba 29-31: Luapula,** Zambia; **Nakuru,** Kenya; **South Rwenzori,** Uganda; **Ibadan-North,** Nijeria; **Connor,** Ireland Yote; **Pusan,** Korea Kusini

### Jumapili 1
Mungu atasuluhisha mizozo ya mataifa atakata mashauri ya watu wengi. Watu watafua panga za vita kuwa majembe, na mikuki yao kuwa miundu ya kupogolea. Taifa halitapigana na taifa lingine wala hayatafanya tena mazoezi ya vita. *Isaya 2:4 (BHN)*

### Jumatatu 2
Tunaomba kwa ajili ya nchi zote katika ulimwengu huu wenye matatizo ambapo vurugu na hofu ni sehemu ya maisha ya kila siku. Tunawaombea waathirika wasio na hatia ambao wamefukuzwa kutoka nyumbani kwao na nchi zao. Tunaombea familia zilizotenganishwa, na watoto ambao wamepoteza wazazi wao na usalama. Bwana wa upendo, bariki wote ambao wangependa kutoa msaada na huduma.

### Jumanne 3
Tunaomba kwa ajili ya wote ambao wana ushawishi wa kimataifa katika biashara, viwanda na uuzaji wa bidhaa.

### Jumatano 4
Tunaomba kwa ajili ya kazi ya Ushirika wa Akina Mama kukuza usalama na elimu kwa wanawake wote. Tunainua kwako Mungu mipango ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote ambayo inasababisha utulivu na maelewano katika jumuiya za wanachama.

### Alhamisi 5
Tunashukuru kwa mashirika yote yanayojaribu kuleta amani duniani; na wale ambao kazi yao ni kupambana na njaa, kuruzuku makazi, kukuza usalama wa chakula na kuhakikisha utoaji salama wa maji safi.

### Ijumaa 6
Yale yanayotokea katika nchi moja yanaweza hatimaye kuleta matatizo kwa nchi zingine nyingi. Basi tunaomba ili viongozi wa kisiasa wafikirie maisha na ustawi wa wote ambao wanaweza kuathiriwa na maamuzi yao. Tupe matumaini ya kweli kwa mustakabali wa amani na uelewano kati ya mataifa yote.

### Jumamosi 7
Ombeni leo kwa ajili ya nchi na wananchi ambao wanateseka, wale walio katika shida, na maangamizi kwa sababu ya vita, majanga, njaa na matokeo yenye athari nyingi kwa ajili ya mabadiliko ya hali ya hewa katika ulimwengu.

### Wimbi la Maombi
**Novemba 2-4: Lebombo,** Msumbiji; **Makueni,** Kenya; **Newala,** Tanzania; **Niger-Delta North,** Nijeria; **Riverina,** Australia na **North East India,** India

**Novemba 5-7: Antananarivo,** Bukini; **Taita Taveta,** Kenya; **Ikara & Ife,** Nijeria na **Argyll & The Isles,** Scotlandi

# Kumbukumbu Novemba 8-14 2020

## Jumapili 8
Nitayakumbuka matendo yako, ee Mwenyezi-Mungu, naam, nitayafikiria maajabu yako ya hapo kale. Nitatafakari juu ya kazi zako, na kuwaza juu ya matendo yako makuu. *Zaburi 77:11-12*

## Jumatatu 9
Baba, asante kwa ajili ya maeneo ya kale ya maombi, kwa kumbukumbu za zamani za kale. Shukrani kwamba imani ambayo ilijiendeleza katika maeneo haya imekuwa ikipitishwa kwa vizazi tangu enzi hizo, na hata leo.

## Jumanne 10
Tunaomba mwongozo kwa ajili ya wazazi wote wa watoto wadogo, kwa sababu kumbukumbu zinazoundwa kwa wakati huu wa thamani ni muhimu na hazitawaondokea kamwe.

## Jumatano 11
Tunapotafakari juu ya maisha yetu, tuna kumbukumbu nyingi ziliochongwa juu ya roho zetu. Tunakushukuru, Bwana, kwa ajili ya zawadi yako ya kumbukumbu na hekima ya miaka. Huku tukikumbuka haya, tunajua kwamba umeshiriki nasi wakati ulio na thamani. Tuendelee kutengeneza kumbukumbu nzuri katika miaka ijayo.

## Alhamisi 12
Mungu mwenye upendo, wakati kumbukumbu zetu bado zina uwezo wa kutuumiza, tusaidie kusamehe, kama vile Kristo anavyotusamehe. Tukikumbuka wakati wa uchungu, tuige mfano wa msamaha wa Kristo; Kumbukumbu na zijae neema yake.

## Ijumaa 13
Tunakumbuka wale ambao wamepoteza kumbukumbu zao kwa njia ya uzee au ugonjwa, na kila mtu ambaye kumbukumbu yake ya zamani ni wazi zaidi kuliko hali halisi ya sasa. Tunaomba ili watunzwe kwa huruma na wawekwe kwa hali ya usalama.

## Jumamosi 14
Furahia kumbukumbu nzuri. Lakini usitumie siku zako zilizobaki hapa kwa kuangalia nyuma, ukitamani "siku nzuri za zamani". *Randy Alcorn, Mwandishi Mkristo Mmarekani*. Bwana, tujaze na shukrani kwa ajili ya siku za nyuma na imani katika mipango yako kwa maisha yetu ya baadaye.

### Wimbi la Maombi

**Novemba 9-11: Kadugli & Nuba Mountains,** Sudan; **Kinkiizi,** Uganda; **Amichi & Igbomina West,** Nijeria na **Ottawa**, Kanada

**Novemba 12-14: Ukhahlamba,** Afrika Kusini; **Maseno West,** Kenya; **Oji River,** Nijeria; **Dunkwa-on-Offin,** Ghana; **Guildford,** Uingereza na **Coimbatore,** India

# Nguvu ya Maombi 15-21 Novemba 2020

## Jumapili 8
Msiwe na wasiwasi juu ya kitu chochote, ila kwa kila hali, mwombeni Mungu katika sala juu ya mahitaji yenu, kwa shukrani. Nayo amani ya Mungu ipitayo akili zote za watu italinda salama mioyo na akili zenu katika kuungana na Kristo Yesu. *Wafilipi 4:6-7*

## Jumatatu 16
Ee Bwana, asante kwa elimu na uhakika kwamba kila sala inatujumuisha kwa uwezo wako. Tunaomba ili uwezo wako wa kubadilisha ufanye kazi ndani yetu kwa kutuwekea changamoto, kutuhamasisha na kutuhimiza kwa matumaini na kujiamini huku tukikuletea maombi yetu.

## Jumanne 17
Ee Bwana, jenga mioyo yetu iwe misafi, mioyo ya kujiamini na ya faraja huku tukishiriki na wewe hofu zetu na mawazo. Tusaidie kusikiliza ufahamu wako wa upendo ili utuongoze kwenye njia sahihi wakati tunapaswa kufanya maamuzi.

## Jumatano 18
Nguvu ya sala sio rahisi kueleza lakini mtu anaweza kupata uzoefu wake. Hebu tumshukuru Mungu leo kwa wakati wote ambapo tumehisi maombi ya wengine wanaotuombea na kuinuliwa kimiujiza katika mikono ya upendo wa Mungu, kwa njia ya maombezi yao kwa niaba yetu.

## Alhamisi 19
Sala sio kushinda  ugumu wa Mungu lakini ni kumiliki nia yake. *Martin Luther*. Mwenyezi Mungu, tunaleta maombi yetu na dua zetu tukitegemea utayari wako wa kutusikia na uwezo wako kwa kutujibu.

## Ijumaa 20
Bwana, tunakuomba utufundishe kujenga matumaini na imani kwa njia ya nguvu ya maombi na furaha na ujasiri tunazopata tunapoendelea kutafuta uongozi wako katika hatua zetu kubadilisha jamii na kuangaza mapenzi yako.

## Jumamosi 21
Mwanga wa Mungu hunizingira; upendo wa Mungu hunizungukia, nguvu ya Mungu hunilinda. Uwepo wa Mungu ni mwangalizi juu yangu. Popote nipo, Mungu yupo!
*James Dillet Freeman, Waziri wa Umoja, aliandika haya 1940 yakiwa maombi ya ulinzi*

### Wimbi la Maombi
**Novemba 16-18:** Iraq; **Katakwa,** Kenya; **Kafanchan & Asaba,** Nijeria; **Lincoln,** Uingereza na Trinidad & Tobago

**Novemba 19-21: Muyinga,** Burundi; **Lake Rukwa,** Tanzania; **Okrika,** Nijeria; **St Asaph,** Wales; **Bendigo,** Australia na **Gujarat,** India

# Haki ya kijinsia

## Novemba 22-28 2020

### Jumapili 22
Chochote kilichofichwa kitafichuliwa, na siri yoyote itagunduliwa na kujulikana hadharani. *Luka 8:17*

### Jumatatu 23
Bwana wa mbingu na ardhi, tunaomba kwamba watu wote wafuate mfano wa kutendea wanawake kwa usawa na heshima ya Kristo. Tunaomba kwa ajili ya mwanzo mpya wa ulimwengu bora ambapo haki na amani zinaweza kunawiri. Amina

### Jumanne 24
Udhalimu wa kijinsia unaathiri zaidi wanawake na wasichana. Wanawake wanakumbwa na ubaguzi nyumbani na katika sehemu wanapoajiliwa. Wanawake ndio kundi kubwa zaidi linaloathiriwa na umaskini duniani. *Side By Side: harakati ya imani kwa haki ya kijinsia*

### Jumatano 25
Tunaomba leo kwa ajili ya mafanikio ya Lengo la Maendeleo Endelevu ili kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote.

### Alhamisi 26
Mungu wa haki, sikiliza sala zetu kwa ajili ya kazi ya wanachama wetu duniani kote, ya kushughulikia madhara ya udhalimu wa kijinsia kwa wanawake na wasichana. Tunaomba ili wajazwe na ufahamu wa kiroho na rasilimali ya vitendo wanapofanya kazi ya kuleta mabadiliko mema.

### Ijumaa 27
Bwana, tusaidie kuchukua hatua, na uamshe mioyo yetu ili tuwakilishe na kuungana kwa ajili ya haki ya kijinsia. Tujenge dunia ya haki iliyojazwa na upendo wako, dunia ambapo ubaguzi unapingwa, ambapo kuna ushirika wa utajiri wa uumbaji, na watu wanaishi kwa amani na heshima.

### Jumamosi 28
Bwana wa upendo, ambaye umetuita kuwa mwili wa Kristo, tutayarishe kuwa kama mikono na miguu katika dunia, ili kuongeza utambuzi wa yale ambayo ni lazima yatolewe changamoto, na kushughulikia hatma ya wale wanaoishi katika mazingira magumu.

### Wimbi la Maombi

**Novemba 23-25: Southern Malawi,** Malawi; **Northern Uganda,** Uganda; **Lafia & Ilaje,** Nijeria na **Thoothukudi-Nazareth,** India

**Novemba 26-28: Zululand,** Afrika Kusini; **Lodwar,** Kenya; **Isiala Ngwa South,** Nijeria; **Accra,** Ghana; **Bangor,** Wales na **Colombo,** Sri Lanka

### Jumapili 29
Watu waliotembea gizani wameona mwanga mkubwa. Watu walioishi katika nchi ya giza kuu, sasa mwanga umewaangazia. *Isaya 9:2*

### Jumatatu 30
Majilio ni maadhimisho ya kuhama kutoka giza kwenda mwangani.  Bwana wa upendo, tunaomba tuwe nuru duniani ambapo wengi bado wapo gizani, kwa kuishi kwa namna ambayo inaonyesha wengine njia zako.

### DESEMBA
### Jumanne 1
Majilio ni wakati wa kusubiri - kusubiri maadhimisho ya kuja kwako kati yetu. Bwana wa wakati na milele, tupe neema ya kusubiri na kutumia vizuri muda huo tunaposubiri. Jaza kusubiri kwetu matumaini tunapojitayarisha kupokea Mtoto Kristo upya, kwa upendo na furaha.

### Jumatano 2
Majilio ni kipawa; wakati wa kutoa na kupokea.  Bwana utupendaye, katika msimu huu wa Majilio tunakuja na mioyo wazi kupokea njia ya kupeana maisha yetu kwa ajili ya Mwokozi wa ulimwengu.

### Alhamisi 3
Katika  shughuli za matayarisho ya Msimu wa Krismasi,  tusaidie kukulenga wewe na kufuata uongozi wako katika maandalizi yetu yote, ili Msimu usiwekwe gizani kwa ajili ya kuweka mkazo wa  kibiashara wakati wa Krismasi. Tunapotayarisha maandalizi yetu ya kimwili, tusisahau kujitayarisha kiroho.

### Ijumaa 4
Kristo Mwokozi wetu, tunaposubiri kusherehekea kuzaliwa kwako mara nyingine Krismasi hii, tunangojea pia kwa hamu kurudi kwako. Ingawa hatuna hakika ni wakati gani, tusaidie kuwa tayari kupokea kuja kwako tena duniani katika utukufu.

### Jumamosi 5
Majilio ni mlango: mahali ambapo kila mtu anakaribishwa. Tunaomba tuwe na hakika ya kukubaliwa tukisimama katika mlango wa Majilio, tukiwa na shukrani rohoni zetu; tayari kuingia upya katika ajabu ya hadithi ya wokovu.

### Wimbi la Maombi
**Novemba 30- Desemba 2: Mpumalanga,** Afrika Kusini; **Buganda ya Kati,** Uganda; **Zonkwa,** Nijeria; **Bo,** Sierra Leone; **Newcastle,** Uingereza na **Barrackpore,** India

**Desemba 3-5: Akot,** Sudan Kusini; **Tanganyika Kusini-Maghari**bi, Tanzania; **Aba & Irele-Ese Odo,** Nijeria; **Coventry,** Uingereza na **Cuttack,** India

# Tangazo Desemba 6-12 2020

## Jumapili 6
Tazama inavyopendeza kumwona mjumbe akitokea mlimani, ambaye anatangaza imani, ambaye analeta habari njema, na kutangaza ukombozi! Anauambia mji wa Siyoni: "Mungu wako anatawala!" *Isaya 52:7*

## Jumatatu 7
Bwana, wakati tunapoyasikia tena maneno ya kinabii ya wajumbe wako walioyasema miaka mingi iliyopita, imani yetu inapata nguvu. Tunakusifu huku tukitafakari ajabu ya kutimika kwa maneno haya, kwa njia ya kuja kwa Masiya wetu, Yesu Kristo.

## Jumanne 8
Sisi kama watu waliobarikiwa na Mungu, tunatangaza utukufu wako. Tutakuwa wajumbe wako ili kutangaza upendo wako na rehema kwa ulimwengu ambao unahitaji Mwokozi.

## Jumatano 9
Sauti zetu hebu zijiunge na Malaika kuimba juu ya upendo wa Mungu kwa ajili ya watu wake, na kutangaza uaminifu wake. Habari njema ambayo itasababisha furaha kubwa kwa ajili ya wote katika kila kizazi. 'Utukufu kwa Mungu juu mbinguni, na duniani iwepo amani kwa wale ambao amependezwa nao'.

## Alhamisi 10
Bwana, nisaidie kunena maneno ya Mungu kwa ujasiri na kwa sauti kubwa leo, ili wengine waweze kusikia Habari yako Njema, ili wapate mwongozo wa kujibu kwa nia.

## Ijumaa 11
Mungu wa wokovu, amsha nafsi zetu; fungua roho zetu tunapojitayarisha kutangaza upya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Sauti zetu ziungane pamoja kutangaza ujio wa Mfalme wa amani.

## Jumamosi 12
Kila sauti itangaze sifa zako na kila mmoja wetu apige magoti mbele yako. Ahadi dhahiri ya imani yetu. Wema wako, kama vazi, utuinue kwa Mungu aliye juu mbinguni. *Jessica Coupé, Mwandishi*

### Wimbi la Maombi

**Desemba 7-9: Namibia; Mount Kenya Kusini,** Kenya; **Northern Izon & Ijebu North,** Nijeria, na **Durham,** Uingereza

**Desemba 10-12: Lusaka,** Zambia; **Shyogwe,** Rwanda; **Sokoto & Ikka,** Nijeria; **Ely** Uingereza na **Karimnagar,** India

# Kusafiri

## Desemba 13-19 2020

### Jumapili 13
Sauti ya mtu anaita jangwani: "Mtayarishieni Mwenyezi-Mungu njia, nyosheni barabara kuu kwa ajili ya Mungu wetu". *Isaya 40:3*

### Jumatatu 14
Bwana wetu Kristo, tunaposafiri kwa mara nyingine tena kwa njia ya Majilio tunashukuru kwamba hatuko peke yetu- tunatembea pamoja na mahujaji wenzetu, tukifurahia upendo wako, tunaposafiri katika maajabu ya kuzaliwa kwa Yesu.

### Jumanne 15
Bwana wa upendo, hata tukiwa tumesafiri njia ya Majilio kwa miaka mingi, tunaomba tuendelee kusisimuliwa na kuburudishwa na njia hii. Tusaidie kuwa tayari kupokea changamoto mpya na mfano wa kuvutia, huku tukipata faraja katika furaha za kawaida.

### Jumatano 16
Bwana Yesu, wakati safari yetu ya Majilio inakuwa ngumu tafadhali tupatie nguvu tunazohitaji ili kushinda vikwazo na matatizo kwenye njia; yawe matatizo ya muda, ya mahusiano au matatizo ya aina nyingine.

### Alhamisi 17
Safari yetu ya Majilio inapofika mwisho, nasi tufikie mahali ambapo Yesu anaishi Bethlehemu, tupige magoti kama Mamajusi, na kumwabudu kama Mfalme wetu pekee na wa kweli. *Mark Zimmerman, Mwandishi*

### Ijumaa 18
Tunapoendelea na safari yetu ya Majilio tuweze kunyoosha njia ambazo zinatupeleka kwenye utukufu wa Bwana. Tunaposafiri ili kumwabudu Mfalme wetu aliyezaliwa, tuchukue kila hatua tukiwa na matumaini na furaha.

### Jumamosi 19
Tunaposhindwa kuona njia mbele, Bwana, tusaidie kukuamini wewe utuongoze kwa njia inayofaa, ili utuonyeshe njia ya kufuata. Uwe kiongozi wetu kupitia Majilio na zaidi, mpaka tufike makao yetu ya milele.

### Wimbi la Maombi

**Desemba 14-16: Fianarantsoa,** Bukini; **Tanganyika ya Kati,** Tanzania; **Calabar & Igbomina,** Nijeria; **Derry & Raphoe,** Ireland Yote, na **Banks & Torres,** Vanuatu

**Desemba 17-19: Lui,** Sudan Kusini; **Embu,** Kenya; **Orlu & Awori,** Nijeria; **The Murray,** Australia na **Medak,** India

# Kuzaliwa kwa Yesu Kristo Desemba 20-26 2020

## Jumapili 20

Walipokuwa huko, siku yake ya kujifungua ikawadia, akajifungua mtoto wake wa kwanza wa kiume, akamvika nguo za kitoto, akamlaza horini kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni. *Luka 2:6-7*

## Jumatatu 21

Tunawaombea wote ambao maadhimisho ya Krismasi ni magumu kwao, wale ambao ni wagonjwa, wakiwa nyumbani au hospitalini, wafiwa, waliopotea na wapweke. Wajue mwanga wa Mtoto Kristo katika maisha yao wakati huu.

## Jumanne 22

Katika ulimwengu huu ulio na shughuli nyingi, Mungu atusaidie kupata muda wa kutafakari juu ya ujio wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Mioyo yetu ifunguke ili kupokea ufahamu safi na kuelewa umuhimu wa Kuzaliwa kwa Yesu.

## Jumatano 23

Asante, Bwana, kwamba tunaweza kupata muda wa kukaa na familia zetu kwa wakati huu maalum wa mwaka. Tunawaombea wale ambao watakuwa peke yao wakati wa Krismasi; wajue faraja ya upendo wako kwenye roho zao.

## Alhamisi 24

Krismasi ni zawadi ya upendo iliyovikwa ndani ya mwili wa binadamu na kufungwa kwa usalama na ahadi imara ya Mungu. Jambo hili haliwezi kuelezeka kwa maneno, kwani ni jambo linalopokewa, kuaminiwa na kueleweka rohoni. *Chanzo hakijulikani*

## Ijumaa 25 Siku ya Krismasi

'Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto wa kiume, na mamlaka itakuwa juu ya mabega yake.' Kwa mshangao na furaha tunasherehekea Kuzaliwa kwa Masiya wetu, Yesu Kristo.

## Jumamosi 26

Tunamsifu Mungu kwa ukweli wa neno lake ambalo linatuvuta kwenye hori la wokovu ulio imara; mahali alipozaliwa Mkombozi wetu katika fahari yake yote isioonekana. Tunapomtazama yule Mtakatifu, maisha yetu yanajazwa na furaha ya upendo wake, zawadi takatifu tunayopaswa kushiriki na watu wa nchi zingine, ili wote waipokee kwa imani yao.

### Wimbi la Maombi

**Desemba 21-23: Maaskofu Wakuu, Maaskofu na makasisi wote katika jumuia ya Anglikana**

**Desemba 24-25: Wakimbizi, familia kimbizi ndani ya nchi zao na wale wanaoishi katika hali ya hofu**

# Kufurahi na Kutafakari Desemba 27-31 2020

## Jumapili 27
Lakini Maria aliyaweka na kuyatafakari mambo hayo yote moyoni mwake. Wale wachungaji walirudi makwao huku wakimtukuza na kumsifu Mungu kwa yote waliyokuwa wamesikia na kuona; yote yalikuwa kama walivyokuwa wameambiwa.. *Luka 2:19-20*

## Jumatatu 28
Kama wachungaji, walishangilia kumuona Bwana, nasi pia tushukuru kwa uwepo wake katika maisha yetu. Kama mwanga wa Malaika uliangaza juu ya wachungaji hao, mwanga wa Kristo uangaze juu ya maisha yetu na kutusaidia kushinda kila pembe za giza zinazodhihirika.

## Jumanne 29
Tunawaombea wale ambao bado hawajamjua Yesu kama Bwana. Tunawaombea wale ambao Krismasi kwao ni sababu nyingine ya kujifurahisha zaidi. Krismasi hii iwe  nafasi ya kuona upendo wako katika maisha yao.

## Jumatano 30
Tunasherehekea pamoja kwa furaha na ushirika kwa wakati huu wa mwaka; tusaidie kushiriki furaha hio na daima kutoa shukrani kwa baraka zetu nyingi. Tunawaombea wale ambao Krismasi kwao ni wakati wa huzuni na upweke.

## Alhamisi 31
Mwaka unapofika mwisho na mwingine kuanza, tunatoa shukrani kwa ajili ya mambo ambayo yamekuwa mazuri, tunatubu yale mabaya ambayo tumefanya. Tunaendelea mbele, katika imani, tukijua kwamba wewe, Bwana, upo nasi kila dakika, kila saa na kila siku.

### Wimbi la Maombi

**Desemba 28-30:** **Wote wanaohusika na wajibu wa kutunza na kusaidia maisha ya familia**

**Desemba 31:** **Ushirika wa Akina Mama kote duniani**

# Sura mpya ya duka la Ushirika wa Akina Mama katika mtandao

## Uchaguzi mpana wa bidhaa zenye alama ya Ushirika wa Akina Mama, beji, machapisho na zaidi. Tunawasilisha kote duniani

www.mueshop.org
























Mothers' UNION
Christian care for families

# Ombi la Mary Sumner

Ee Bwana, siku ya leo,
nisaidie kugusa maisha mengi
iwezekanavyo kwa ajili yako;
na kila maisha nitakayogusa,
roho wako iyahuishe, iwe ni
kupitia neno nitakalosema,
sala ninayopumua,
au maisha ninayoishi.
Amina.

Mothers' UNION
Christian care for families